# Nipashe

Jumanne Juni 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580976

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

JACKPOT BABA LAO!

TZS. 253,545,950

CHEZA SASA KWA 1000/= TU!

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Matamanio** ya Watanzania bajeti 2022/23 haya...

UKURASA 4




**KOCHA SENEGAL ATAKA MANE AJIUNGE BAYERN**

UKURASA 22

# MTAFARUKU KKKT

• **Mapya** ya kugombea mali yaibuka, polisi yawatia mbaroni viongozi... *Endelea ukurasa 2*



Waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Ruanda jijini Mbeya wakiwasikiliza maaskari ambao walienda kusimamia amani baada ya kutokea vurugu kanisani hapo kati ya waumini wa kanisa hilo na mabaunsa waliotaka kulifunga kanisa hilo jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### UAMUZI MDOGO KESI KINA MDEE SASA JUNI 22



MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam inatarajia kutoa uamuzi mdogo wa mapingamizi yaliyowasilishwa na mawakili wa Chama cha...

## Wanaoishi milimani Mwanza kupisha wawekezaji

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na Kiongozi Mkuu wa Oman, Sultan Haitham bin Tariq Al Said, baada ya mazungumzo yaliyofanyika Al Alam Muscut jana. **PICHA: IKULU**

## Aliyeng'olewa umeya Moshi agombea tena



UKURASA 2

MICHEZO PHIRI, SIMBA IMEISHA HIYO UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati), akizindua ripoti ya ushiriki wa makundi maalum katika manunuzi ya umma, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtafaruku mpya kanisa KKKT

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SIKU chache baada ya kuwekwa wakfu kwa Askofu mpya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Dayosisi ya Konde, Geofrey Mwakihaba, pande mbili zinazohasimiana zimeingia kwenye mtafaruku mpya wa kugombea mali za kanisa.

Mtarafuku huo ulijitokeza juzi wakati wa Ibada ya Jumapili Kanisa la KKKT Ruanda, jijini hapa, mahali alipohamishia makao makuu ya Dayosisi ya Konde, aliyekuwa Askofu wa Kanisa hilo, Dk. Edward Mwaikali.

Hali hiyo ilisababisha Jeshi la Polisi kuwakamata viongozi wa kanisa hilo na kuwasweka mahabusu. Waliokamatwa katika sakata hilo ni aliyekuwa Mkuu wa Jimbo la Mbeya Mashariki, Nyibuko Mwambola na Dk. Mwaikali, ambao walipelekwa mahabusu wanakoendelea kushikiliwa.

Kabla ya kukamatwa kwa viongozi hao, Mchungaji Mwambola akiwa madhabahuni alitoa taarifa kwa waumini wa kanisa hilo kuhusu uamuzi wao wa kujitenga na Kanisa la KKKT na kujiunga na Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki.

Hata hivyo, muumini mmoja alisimama na kuhoji uhalali wa uamuzi huo, ndipo alipochukuliwa na viongozi hao na kumwingiza kwenye gari na kutaka kuondoka naye kusikojulikana kabla ya mtu huyo kuokolewa na askari wa Jeshi la Polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ulrich Matei, alithibitisha kukamatwa kwa viongozi hao na kuwekwa mahabusu.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa njia ya simu jana, Kamanda Matei alisema kwa kifupi kuwa wanawashikilia viongozi hao kwa ajili ya mahojiano zaidi.

"Ni kweli tunawashikilia Mchungaji Mwambola na aliyekuwa Askofu wa Dayosisi ya Konde, Dk. Mwaikali kwa mahojiano zaidi, kwa sababu tunatambua kuwa mgogoro wa Dayosisi hiyo ulikwisha baada ya kusimikwa kwa askofu mwingine, lakini inaonekana wao bado wanaendelea na mgogoro huo," alisema Matei.

Wakati hayo yakijiri, uongozi mpya wa Dayosisi ya Konde chini ya uongozi wa Askofu Mwakihaba, unadaiwa kuwatuma mabaunsa pamoja na madalali wa Mahakama, kufunga ofisi zilizokuwa zikitumiwa na uongozi uliopita wa Dk. Mwaikali zilizopo kwenye Kanisa la Usharika wa Ruanda.

Hatua ya kufungwa kwa ofisi hizo, ilisababisha waumini wa kanisa hilo, hasa wanaoaminika kuwa ni wafuasi watiifu wa Dk. Mwaikali, kukusanyika kuzuia uongozi mpya kufanya shughuli zozote ndani ya kanisa hilo kwa madai kuwa wao bado wanamtambua Dk. Mwaikali kuwa ndiye askofu wao.

Mvutano huo wa waumini wa KKKT, ulisababisha Jeshi la Polisi kufika kanisani hapo ili kuwatawanya wafuasi wanaoendelea kumtambua Dk. Mwaikali kuwa ndiye askofu wao, na kupinga hatua iliyofanywa na viongozi wanaodaiwa kuwa wa askofu mpya kufunga kanisa hilo ili kulinda mali zote za kanisa zisitumiwe na askofu aliyevuliwa madaraka.

Mkuu wa Operesheni ya Jeshi la Polisi Mbeya Mjini, Johanes Bitegeko, aliwaamuru waumini waliozingira kanisa hilo kutawanyika mara moja kwa kile alichoeleza kuwa wanafanya mikusanyiko isiyokuwa rasmi.

Aliwataka waumini hao kuwa watulivu wakisubiri maamuzi kutoka mamlaka husika kutoa maelekezo ya kumaliza mgogoro huo ambao umedumu takribani miaka miwili sasa.

"Mgogoro huu bado unashughulikiwa, nawataka waumini kuwa watulivu, sisi kazi yetu ni moja tu kulinda usalama wa raia na mali zao na nyie mmekusanyika hapa bila sababu ya msingi, ondokeni mkaendelee na shughuli nyingine za uzalishaji mali na mambo mengine ya msingi kwa sababu mgogoro huu hautatuliwi chumbani, maamuzi yatakapotolewa kila mtu atajua na huduma zitaendelea, tunaomba muondoke," aliamuru Afande Bitegeko.

Dalali wa Kampuni ya Pamoja Auction Mart, aliyehusika kulifunga kanisa hilo, Lwitiko Mwamaso, alisema uongozi mpya chini ya Askofu Geofrey Mwakihaba, ulimwagiza kwenda kufunga ofisi za kanisa hilo, baada ya aliyekuwa Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Mwaikali kutangaza Usharika wa Ruanda kujiunga na Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki.

Alisema tayari kanisa hilo limejiunga na kanisa jipya na kuamua kubadilisha bango kutoka Kanisa la Kuu la KKKT Dayosisi ya Konde Ruanda na kuweka linalosomeka 'Kanisa la Kilutheri la Afrika Mashariki'.

Emmanuel Mwaisanga, kutoka Usharika wa Sinai jijini Mbeya, alisema ameshtushwa kuona usharika wa Ruanda umejitenga na kuanzisha kanisa lao na kwamba hawako tayari kuona usharika huo unajitenga kwa sababu ni watoto wa baba mmoja.

"Hakuna mtu atakayesimama na kusema amejenga usharika huo wa Ruanda bali kila mwana KKKT kote nchini alishiriki aidha kwa sadaka au njia nyingine kujenga, sio sawa waumini hao kuanza kujimilikisha kanisa hilo na kudai ni mali yao na kuanzisha kanisa lao," alisema Mwaisanga.


**NKAYA COMPANY LIMITED**

*Dealers in: General Auctioneers, Legal Services, Debt Collection, Banking Consultant, Court Brokers, Commission Agent, Estate Agents,*
*P.O .Box 4042,Dar es Salaam. Mob: 0626 180 070; 0717 208 108*
*Email:nkayacompanylimited@yahoo.com*
*Office location: Morgan House, Ground floor, Kimweri Road, Msasani-Dar Es Salaam*

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**NOTISI YA KULIPA DENI NDANI YA SIKU ISHIRINI NA MOJA [21], AU MALI ZILIZOWEKWA KAMA DHAMANA ZITAUZWA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **KCB BANK TANZANIA,** wadaiwa wa dhamana zifuatazo wanatakiwa walipe madeni yao ndani ya siku **ISHIRINI NA MOJA[21]** kutokea tarehe ya kutoka kwa hili tangazo.Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kuuzwa kwa mali walizo ziweka kama dhamana.

| MAELEZO KUHUSU DHAMANA | USAJILI WA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA | TAREHE NA MUDA |
|---|---|---|---|
| NYUMBA NZURI YA KUISHI | CT NO.50407, LO NO.405866, KIWANJA NAMBA 486, KITALU "V". | ILIYOPO ENEO LA NGOKOLO MANISPAA YA SHINYANGA. | 25/07/2022 SAA 06:00 MCHANA |
| NYUMBA NZURI YA KUISHI | CT NO.26823, LO NO. KIWANJA NAMBA 1342, KITALU "TT" | ILIYOPO ENEO LA LUBAGA MANISPAA YA SHINYANGA. | 25/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI |
| NYUMBA NZURI YA KUISHI | CT NO.108989, LO NO.3523815, KIWANJA NO.148, KITALU'19' | ILIYOPO ENEO LA KIBADA MANISPAA YA TEMEKE. | 14/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI |
| NYUMBA NZURI YA KUISHI | CT NO.31237, LO NO.383235 KIWANJA NAMBA.54, KITALU"KKK". | ILIYOPO ENEO LA SHIRIMATUNDA MANISPAA YA MOSHI. | 09/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI |
| KIWANJA CHENYE JENGO KUBWA LA KUHIFADHIA MIZIGO PAMOJA NA OFISI | CT NO.1169, LO NO.44116, KIWANJA NAMBA.6/8, KITALU "C". | ILIYOPO ENEO LA UNGALIMITED JIJINI ARUSHA. | 06/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI |
| SHAMBA LENYE NYUMBA NZURI YA KISASA YA GHOROFA MOJA | CT NO.20131, LO NO.250872, SHAMBA NAMBA 1983 | ILIYOPO KIJIJI CHA OLOIRIEN, KATA YA ARUMERU JIJINI ARUSHA | 20/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI |
| NYUMBA NZURI YA KUISHI | , KIWANJA NO.5/359 USAJILI NO.398 | ILIYOPO ENEO LA MWEMBELADU,WILAYA YA NGA'MBO, ZANZIBAR | 30/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI |
| NYUMBA NZURI YA KUISHI | KIWANJA NO.26/511, USAJILI NO.293 | ILIYOPO ENEO LA KWALAMSHA, WILAYA YA MJINI, ZANZIBAR | 30/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na asilimia 75% atatakiwa kumaliza ndani ya siku kumi na nne (14) endapo atashindwa kulipa kwa muda huo uliowekwa, pesa aliyolipa haitarudishwa na mnada utarudiwa.
2. Ukaguzi wa dhamana zinazofanyiwa mnada utafanyika siku ya mnada.
3. Gharama za kuhamisha mali au kumtoa mtu ndani pamoja na kubadilisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.
4. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
5. Endapo yeyote atajitokeza kuharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kulazimika kulipa gharama za mnada.
6. Dalali wa mnada ni Nkaya Company Limited ndio wenye mamlaka na maamuzi ya mwisho ya kumtangaza mshindi.

**NKAYA MOB:** 0626180070
0717208108
0788448341
0753000825

216901301


# Aliyeng'olewa umeya Moshi agombea tena

**Na Mary Mosha** MOSHI

KINYANG'ANYIRO cha kuwania nafasi ya umeya katika Manispaa ya Moshi kimechukua sura mpya, baada ya jana meya aliyeng'olewa katika nafasi hiyo, Juma Raibu, kuchukua fomu.

Raibu aling'olewa katika wadhifa huo Aprili 11, mwaka huu, baada ya madiwani kupiga kura za siri na kati ya kura 28 zilizopigwa, 18 zilikataa kuendelea na wadhifa wake, huku 10 zikimtetea abaki katika nafasi hiyo aliyodumu nayo tangu ulipofanyika Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Tuhuma zilizomng'oa Raibu ni madai ya kuhudhuria sherehe ya kijana mmoja anayedaiwa kushiriki mapenzi ya jinsia moja, kutumia vibaya ofisi yake, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuruhusu ujenzi holela na kutumia fedha nje ya utaratibu.

Jana, Raibu aliwasili katika ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM) Moshi Mjini majira ya saa sita mchana na kuchukua fomu ya kugombea nafasi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu hiyo, Raibu alisema ameamua kurudi kuwania nafasi hiyo kwa kuwa tangu ameondolewa kwenye nafasi hiyo, anaona Moshi imepoa na kuwapo kwa vurugu nyingi.

"Moshi imelala, sio Moshi niliyokuwa nikiiongoza, nimeona ni wakati wa kurudi kuchukua nafasi hii, ninaamini tutashirikiana na madiwani katika kuiendeleza Moshi," alijitapa.

Alisema zaidi ya wananchi 500 wamefika nyumbani kwake kumuomba na kumchangia ili aweze kurudi kugombea nafasi hiyo.

"Niliwakatalia wananchi na kutaka kupeleka fedha hizi kutoa sadaka, lakini walikataa wakataka nije nichukue fomu na niwaambie nipitishwe au nisipitishwe, nitaendelea kuwa mwanachama wa CCM."

**TISA WAJITOKEZA**

Akizungumza na Nipashe kuhusu mchakato huyo, Katibu wa CCM Moshi Mjini, Ibrahim Mjanakheri, alisema tangu kuanza mchakato wa utoaji fomu Juni 12, tayari madiwani tisa wamechukua fomu.

"Ni kweli umeanza mchakato wa kutafuta Meya wa Manispaa ya Moshi, tayari baadhi ya madiwani wameshachukua fomu akiwamo Apaikunda Nabuli, Francis Shio, Zubery Kidumo, Charles Lyimo, Stuart Nkinda, Charles Mmbando, Nasibu Mariki na Juma Raibu, zoezi hili tunatarajia kulifunga rasmi jioni saa kumi alasiri," alisema Mjanakheri.

Naibu Meya wa Manispaa ya Moshi, Stuart Nkinda, alisema amechukua fomu na yupo tayari kuwania nafasi hiyo.

"Hii nafasi imetangazwa, nimekuwa nikiikaimu, hivyo nimejipima na kuona naweza kuongeza kwa kuzingatia miongozo kanuni na taratibu zilizopo, ni kweli nimechukua fomu".

## Uamuzi mdogo kesi kina Mdee sasa Juni 22

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam inatarajia kutoa uamuzi mdogo wa mapingamizi yaliyowasilishwa na mawakili wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) dhidi ya kina Halima Mdee na wenzake Juni 22, mwaka huu.

Maombi hayo yaliletwa mahakamani na wabunge 19 waliovuliwa uanachama wa chama hicho, wakiongozwa na Mdee.

Pia, Mahakama Kuu siku hiyo itasikiliza maombi mengine ya kuiomba mahakama hiyo iweke zuio la kutokuchukuliwa kwa hatua zozote dhidi yao, hadi pale maombi yao ya msingi yatakapoamuliwa.

Mdee na wenzake walifungua maombi hayo mahakamani hapo kwa nia ya kuiomba itoe kibali cha wao kufungua kesi ya kupinga mchakato wa kuvuliwa uanachama.

Akiwasilisha hoja za pingamizi hilo, mbele ya Jaji Mfawidhi John Mgeta, Wakili Peter Kibatala, alidai maombi hayo yanadosari mbalimbali za kisheria ikiwamo hati ya kiapo iliyounga mkono maombi hayo.

Kibatala alidai miongoni mwa dosari hizo ni hati zote za viapo 19 kusainiwa na waleta maombi pamoja na mawakili wao wakati sheria inataka kiapo kisainiwe na muapaji pekee.

Kibatala alidai kuwa wakili ana sehemu yake ya kusaini, kitendo cha mawakili kusaini katika viapo hivyo wanajimilikisha maelezo ambayo ni ya kuambiwa.

Katika hoja nyingine Kibatala alidai kuwa waleta maombi wameishtaki Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA badala ya wadhamini waliosajiliwa.

Kwa upande wake Wakili Jeremia Mtobesya, ambaye aliiwakilisha CHADEMA aliiomba mahakama kutupilia mbali maombi ya wabunge hao 19 kwa kuwa katika maombi hayo wameishtaki Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambayo haikutakiwa kushtakiwa katika shauri hilo.

Alidai kuwa NEC, haikutakiwa kuunganishwa katika shauri hilo kwa kuwa mahakama haina mamlaka kisheria ya kuhoji maamuzi yake kwa mujibu wa ibara ya 74 (12) ya Katiba ya nchi.

Akijibu hoja za pingamizi hilo, Wakili Aliko Mwamanenge kwa niaba ya wabunge hao, aliiomba mahakama itupilie mbali mapingamizi hayo kwa sababu hoja zao hazina msingi wowote.

Akizungumzia hoja ya kwamba mahakama hiyo haina mamlaka kuchunguza maamuzi ya NEC, Wakili Mwamanenge alidai katika shauri hilo hawajaiomba mahakama ifanye uchunguzi wowote kwa kile ambacho NEC imefanya na mahakama ina haki ya kuruhusu maombi yao.

Alidai kuwa katika kesi hiyo NEC bado haijataja majina au kuchagua wabunge wengine wa kujaza nafasi za wabunge hao, waleta maombi wanachotaka kuzuia NEC isifanye chochote kwa sasa.

Kwa upande wake Wakili Ebson Kilatu ambaye naye aliwawakilisha wabunge hao akizungumzia hoja ya kuishtaki Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA, alidai ni sahihi kwa kuwa ndicho chombo kinachofanya maamuzi ya chama.

Kuhusu hoja ya mawakili kusaini katika viapo hivyo, wakili Kilatu alidai hawajasaini katika viapo hivyo bali waliandika tarehe ya uandaaji viapo hivyo na kusaini eneo hilo, haiathiri hoja za maombi hayo.

# Wanaoishi milimani Mwanza kuondolewa

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAKAZI wa Jiji la Mwanza waliojenga maeneo ya milimani wanatarajiwa kuondolewa ili kupisha wawekezaji kutoka nchini Brazil.

Wawekezaji hao wanatarajia kuwekeza kwenye sekta ya miundombinu, viwanda na utalii katika maeneo ya Igogo, Isamilo na Kegeto.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake hivi karibuni, Meya wa Jiji la Mwanza, Sima Constantine, alisema mpango huo unalenga kuboresha miundombinu pamoja na kukuza sekta ya utalii utakaogharimu Sh. bilioni 150.

Alisema makubaliano hayo yanahusisha wawekezaji kutoka nchini Brazil katika Jiji la Rio de Janeiro, ambao walifika jijini humo, kuangalia fursa za uwekezaji katika miundombinu, viwanda na utalii.

Costantine alisema maeneo mengine ambayo wawekezaji hao wanayalenga ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha pembejeo za kilimo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Kanda ya Ziwa.

"Sehemu zingine ni ujenzi wa barabara pamoja na nyumba za ghorofa katika milima mbalimbali ambayo inaangalia ufukwe wa Ziwa Victoria," alisema.

Alitaja sehemu zingine watakazozigusa kuwa ni pamoja na kutengeneza eneo la ufukwe wa Ziwa Victoria sehemu ya kliniki, Nera jirani na kituo cha polisi wa majini ambalo litatengenezwa na kuwa sehemu za uwekezaji na utalii.

Constantine alisema mpango huo utasaidia ukuaji wa uchumi wa Jiji la Mwanza na mtu mmoja mmoja.

Alisema wawekezaji hao wana umoja wao nchini Brazil unaojulikana kama 'Africa Unity' na mpaka sasa wamewekeza nchini Dubai na Ethiopia.

Aliongeza kuwa katika makubaliano ya mpango huo, Jiji la Mwanza litatoa ardhi na wawekezaji watatoa mtaji, teknolojia na mradi huo utakapokamilika utanufaisha pande zote mbili.

**ULIPAJI FIDIA**

Akizungumzia uwekezaji wa maeneo ya milimani, Constantine alisema, jiji limepewa jukumu la kulipa fidia katika maeneo ya Igogo, Isamilo na Kegoto ambayo yapo mlimani ili kupisha uwekezaji huo.

Constantine alisema wawekezaji hao wamekubaliana na jiji litafute ardhi na kukamilisha mipango yote ndani ya miezi mitatu kuanzia mwanzoni mwa mwezi huu kabla ya kazi hiyo kuanza.

Aliongeza kuwa wawekezaji hao wanaendelea kutafuta maeneo mengine ya kuwekeza ikiwamo mikoa ya Dodoma na Arusha.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (katikati), akitoka kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana, baada ya kufunga zoezi la bure la upimaji wa afya kwa mkoa wa Dar es Salaam. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Health Sciences (HASAFA), Kapil Bhandari na Mtangazaji wa Clouds, Sebastian Maganga (kushoto). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Walinzi wasimulia padri aliyeuawa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU moja baada ya mwili wa Padri wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (White Fathers), Michael Samson (63), kuokotwa akiwa amefariki, walinzi wa kituo alichokuwa akihudumia wameeleza namna alivyowaaga kabla ya kufikwa na umauti.

Padri Michael alikutwa amefariki kwenye Mto Meta chini ya Daraja la Sabasaba jijini hapa, huku mwili wake ukiwa umekatwa viungo na kutenganishwa. Akizungumza na Nipashe mmoja wa walinzi wa Kituo cha Vijana cha Kanisa Katoliki Mbeya alikokuwa akiishi, Theresia Mwela, alisema Padri Michael ndiye aliyekuwa Mkurugenzi wa Kituo hicho na walikuwa wanaishi naye vizuri muda wote na hakuwahi kuwa na tatizo lolote.

Alisema kiongozi huyo alikuwa na utaratibu wa kuaga kila siku jioni akiwaeleza kuwa anakwenda kufanya mazoezi ya kutembea na kila baada ya mazoezi alikuwa akirejea na kutoa taarifa kuwa amerudi.

Mwela alisema kuwa siku ya Ijumaa alipoondoka kwa mara ya mwisho alitoa taarifa, lakini walishangaa kutorejea kama ilivyo kawaida yake mpaka siku iliyofuata walipopata taarifa kuwa mwili wake umeokotwa chini ya daraja ukiwa umecharangwa mapanga.

"Father mwenzake aliyekuwa anakaa naye alikuja na gari akasema anamtafuta hamuoni na mimi nikamweleza kwamba hajarudi, baada ya hapo aliondoka lakini kesho yake akaja akatuambia kwamba Father Samson ametutoka," alisema Mwela.

Alisema pamoja na kuwa kiongozi Mkuu wa Kituo hicho, alikuwa mtu wa kujishusha na kuwasalimia watu wote wanaofanya kazi kituoni hapo.

Mwela alisema kiongozi huyo alikuwa mstaarabu na hakuwahi kuwa na makundi ya aina yoyote ambayo pengine yangehisiwa kuwa ni hatari kwa maisha yake.

Hata hivyo, uongozi wa kanisa hilo haukupatikana kutoa taarifa ya utaratibu wa mazishi ya Padri Michael, huku taarifa zikieleza kuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Mbeya, Gervas Nyaisonga alikuwa safarini.

Juzi Jeshi la Polisi kupitia Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, Ulrich Matei, lilitoa taarifa kuwa linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ikiwa ni pamoja na kujua chanzo cha mauaji hayo, huku likilaani mauaji hayo.




Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, akizungumza na wamachinga kuhusu huduma mbalimbali za Benki ya NMB baada ya kuzindua promosheni ya Teleza Kidigitali kwenye stendi ya mabasi CDT katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama. Promosheni hiyo imelenga kutoa elimu kwa wateja na Watanzania kwa ujumla kuhusu huduma za Benki ya NMB kama Mshikofasta, NMB pesa wakala na Lipa mkononi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watalii wafurika Serengeti, Ngorongoro

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WADAU wa utalii wamesema kwa sasa kuna mafuriko ya wageni hali iliyosababisha hoteli za Serengeti na Ngorongoro kujaa, ikiwa ni matokeo ya Royal Tour na kulegezwa kwa masharti ya UVIKO-19 kulikowezesha wageni wengi kusafiri.

Hata hivyo, wameiomba serikali kukaa na wadau kujadili mikakati ya kupanua uwekezaji kwa kuwa mwakani mafuriko yatakuwa mengi zaidi kutokana na filamu ya Royal Tour kuitangaza Tanzania na kutengeneza sababu ya kwanini mgeni aje nchini.

Mwenyekiti wa Chama cha Waongoza Watalii Tanzania (TATO), Wilbad Chambulo, alisema kwa msimu huu ulioanza mwishoni mwa Machi, mwaka huu, wamepokea wageni zaidi ya 300,000 kutoka Ulaya na 50,000 Marekani, na kwamba kwa sasa hakuna nafasi kiasi cha kulazimika kuwaomba wateja kusogeza mbele safari zao.

"Pia kwa saa tumepokea mchanganyiko wa wageni kutoka masoko mapya tofauti na miaka mingine kama Ufaransa, Italia, Dubai, Uturuki pamoja na Spain ambalo ni soko la muda mrefu.

"Watalii wanaotumia fedha nyingi ni kutoka Ulaya ikilinganishwa na mabara mengine, lakini ni karibu kwa kuwa ni saa nane tu hadi nchini, huko nyuma tulikuwa na wageni wengi kutoka Urusi na Ukraine, lakini kwa sababu ya vita hawaji," alisema.

Alisema kwa miaka miwili 2020/2021 hawajafanyakazi kutokana na UVIKO-19, na kwamba Royal Tour imechagiza wageni wengi kuja nchini ambako tahadhari zote za ugonjwa huo zimechukuliwa.

"Kwa sasa wageni wote wamechanja na wafanyakazi wa sekta wamechanja, Rais Samia Suluhu Hassan, ametusaidia na kwenda kufungulia maji kwenye bomba kubwa la Royal Tour, upande wa serikali wanatusaidia sana kutokana usumbufu wa wageni haupo, watendaji wanaelewa maana ya utalii ndiyo maana wanamiminika kwa sasa," alibainisha.

Kwa mujibu wa Chambulo ambaye ni mwekezaji mkubwa wa hoteli za nyota tano nchini kwenye vivutio vya utalii nchini, alisema "Booking (nafasi) zimejaa, tumejaza hoteli kwa kweli sasa tunafanya kazi tunafidia tulichopoteza kwa miaka miwili, labda litokee jingine kama sasa vita inachangia mafuta kupanda bei maana yake vitu na nauli hata za ndege zitapanda bei."

Alisema sekta binafsi imejiandaa kikamilifu, lakini inahitaji ushirikiano mkubwa wa serikali kwa kuwa kwa miaka mwili hawajawekeza na sasa matokeo makubwa ya Royal Tour yataonekana mwaka 2023 kuendelea, lazima tujipange sasa kujadiliana kuondoa changamoto zinazokwaza uwekezaji kwenye sekta hiyo.

"Sisi tunawekeza fedha na mali, serikali itusaidie kupunguza vikwazo, tukae nao tuangalie tutawezaje kupokea wageni milioni tano, tuwe na sehemu za malazi za kutosha, utalii tunauza bidhaa ambayo inahitaji maandalizi ya mapema kwa kuwa wengi hukusanya fedha na kutafuta pa kwenda kuzitumia," alisema Chambulo.

"Mfano kwa sasa wageni wanaomba kuja tunawaambia itabidi wakae kwenye 'tent' au camp maalum maana hatuna vyumba vya kuwaweka, wapo wanaomba kuja hivyo hivyo na kuishi kwenye camp wanafanya utalii na kuondoka, mimi hoteli zangu zote kuanzia Burunge, Serengeti na Ngorongoro zimejaa wageni hadi wanaomba sasa nawaambia wasubiri kwanza," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema; "mwakani hali itakuwa nzuri zaidi kama watendaji watamwelewa Rais na kushirikiana nasi, lazima tukae pamoja tuweke malengo na mikakati ya kuyafikia kwamba mafuriko ya wageni tunayamudu vipi."

Naye Katibu Mtendaji wa Shirikisho la Vyama vya Utalii 12 Tanzania, Richard Rugimbana, alisema wageni wameongezeka na kwamba mwakani kutakuwa na mafuriko zaidi na watu wanafanyakazi tofauti na mwaka 2020/21 walifunga biashara, wafanyakazi kwenda likizo za lazima na walipokea wageni 600,000 waliokuwa wameweka nafasi robo ya kwanza kabla ya Machi.

"Safari kubwa ya impact (matokeo) ya Royal Tour ni mwaka 2023/24, kwa sasa ni dalili nzuri sana. Tuna mafuriko Serengeti na Ngorongoro kumejaa huwezi kwenda ukapata chumba labda uwe ulifanya booking (nafasi) mapema," alisema.

"Royal Tour ya Rais Samia ameenda nje kuamasha utalii wa Tanzania ni mwema ni mzuri tunawakaribisha mje mtembelee, kuna umuhimu wa sisi kuja na mkakati wa utalii wa ndani ya nchi kuanzia miundombinu ya viwanja vya ndege, hoteli. Pia tuwe na wa Afrika Mashariki ili tuwapokee wageni wote na kuendelea kuwa kitovu cha utalii," alisema.

Juni 4, mwaka huu, kwa mara ya kwanza kampuni ya watalii duniani ya Eurowings Discovery ilitua katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), ikiwa na watalii 130 waliokuja kutembelea vivutio mbalimbali kama Mlima Kilimanjaro, Zanzibar, Serengeti na Ngorongoro.

Akizungumza wakati wa kupokea ndege hiyo, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema kuja kwa ndege hiyo ni heshima na jambo muhimu kwa sekta ya utalii, huku Mwenyekiti wa Bodi ya KADCO, Dk. Natu Mwamba, akisema filamu hiyo imeongeza ujio wa watalii na wawekezaji nchini.

"Ujio wa ndege hiyo ni chachu ya kuongeza wasafiri na watalii ambao itaendana na lengo la serikali kufikia watalii milioni tano, mwaka 2025," alisema.

Wiki iliyopita, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alilieleza Bunge kuwa kwa sasa kuna mafuriko ya watalii huku akisema mji wa Karatu umepokea wageni wengi kuliko miaka mingine, kichocheo kikubwa ni filamu ya Royal Tour.

# Matamanio ya Watanzania bajeti mwaka 2022/23

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MATAMANIO ya Watanzania kuhusu kushuka kwa bei ya mafuta nchini, yatakayoleta unafuu wa maisha yanatarajiwa katika bajeti ya serikali itakayowasilishwa bungeni leo.

Bajeti ya mwaka 2022/23, ambayo pamoja na kuonyesha mwelekeo wa nchi hasa kwenye vyanzo vipya vya mapato, matarajio ni kujua kodi zitakazoondolewa kwenye mafuta.

Mei, mwaka huu, Rais Samia alikutana na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba na Waziri wa Nishati, January Makamba, na viongozi wengine walielekeza kutolewa kwa Sh. bilioni 100 kupunguza makali, huku hatua zaidi za kikodi kujulikana wakati wa bajeti.

Juni mosi, mwaka huu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilitangaza bei kikomo kuwa lita moja ya petroli kuuzwa Sh. 2,994 na dizeli Sh. 3,131, baada ya serikali kuweka ruzuku ya Sh. bilioni 100 kwenye mafuta.

**TOZO/KODI**

Hadi sasa tozo zinazotozwa kwenye mafuta ni ya matumizi ya miundombinu ya bandari inayotozwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), kuchakata nyaraka za forodha ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kupima na kuthibitisha kiwango cha mafuta kinachopokelewa chini ya Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA).

Kupima na kuthibitisha ubora wa mafuta ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), uwakala wa Meli ya Shirika la Wakala wa Meli (TASAC) na ya shughuli za udhibiti wa biashara ya mafuta ya EWURA.

Aidha, tozo za taasisi za serikali ni matumizi ya bandari, huduma kwenye halmashauri, tozo katika biashara ya jumla na rejareja kwa wakaguzi wa miundombinu, Baraza la Mazingira Tanzania (NEMC), OSHA, Zimamoto, Wakala wa Barabara Tanzania (TANDROADS), Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA).

Mei 10, mwaka huu, Waziri wa Nishati, aliwasilisha bungeni hatua zilizochukuliwa na serikali ili kuleta nafuu, huku ahidi kubwa ikisubiriwa kwenye bajeti ya serikali.

Hivi karibuni, wachumi, wasafirishaji na wananchi walisema ruzuku ya serikali imeleta nafuu ndogo, na sasa wanasubiri kuondolewa kwa kodi zilizoko ambako kutaleta nafuu ya bidhaa hiyo na kushusha bei ya bidhaa.

Msemaji wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA), Mustapha Mwalongo, alisema hatua ya ruzuku ya bilioni 100 ni nzuri imeleta unafuu kwenye bei ya bidhaa hiyo, na kwamba wanasubiri hatua za kikodi ambazo zitapunguza zaidi.

"TABOA tunasubiri kwa hamu kwamba bajeti kuu inaweza kuondoa kodi nyingi, inawezekana itasaidia kama alivyotoa ushauri Rais," alisema msemaji huyo.

Mhadhiri wa Uchumi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Razack Lokina, alisema jitihada za serikali ni nzuri ingawa zinasubiriwa za bajeti ya serikali.

Alisema mafuta yakipanda yanachangia mfumuko wa bei, hatua ya serikali ilikuwa ni sawa, bila hivyo yangeendelea kuwa juu zaidi, gharama ya maisha ingekuwa kubwa licha ya kwamba mishahara bado haijaongezeka.

Mwenyekiti wa waendesha Bajaji wenye ulemavu, Dar es Salaam, Paul Masamaki, alisema wanasubiri kwa hamu bajeti itakayoondoa kodi kwenye mafuta na kuleta unafuu mkubwa.

**BAJETI 2022/23**

Machi 12, mwaka huu, Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, akiwasilisha bungeni ukomo wa bajeti, alisema serikali imepanga kutumia Sh. trilioni 41.063 kwa mwaka wa fedha 2022/23, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na bajeti ya Sh. trilioni 37.980 mwaka 2021/2022.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. trilioni 25.542 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni asilimia 62.2 ya bajeti yote, ikiwa ni Sh. trilioni 11.308 kwa ajili ya ulipaji deni la serikali na gharama.

Alisema matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 15.521 sawa na asilimia 37.8 ya fedha yote, kati yake Sh. trilioni 12.122 fedha za ndani na Sh. trilioni 3.399 ni fedha za nje.

HABARI KITAIFA

# 10 mbaroni tuhuma kuhusika na kifo cha askari Loliondo

**Na Thobias Mwanakatwe,** ARUSHA

WATU 10 wamekamatwa na Jeshi la Polisi wakituhumiwa kuhusika na vurugu zilizojitokeza wakati wa uwekaji wa mipaka kwenye eneo la pori tengefu la Loliondo, wilayani Ngorongoro, mkoani hapo.

Akizungumza na Nipashe Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, alisema watu hao wamekamatwa katika operesheni inayoendelea kufanywa na jeshi hilo.

Katika vurugu hizo askari namba G4200 mwenye cheo cha Koplo, Garlus Mwita Garlus, ambaye alikuwa akifanyakazi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dodoma aliuawa kwa kuchomwa mshale.

Kamanda Sabas alisema: "Tumewakamata watu 10 na hii operesheni itakuwa endelevu hadi tuhakikishe wote waliohusika wanatiwa mbaroni."

Kamishna Sabas juzi wakati wa kuaga mwili wa askari wilayani aliyeuawa kwa kuchomwa mshale Loliondo, alisema watu wote walioratibu, kushiriki mauaji ya askari watakumbana na mkono wa dola.

"Yeyote aliyeshiriki kupanga, kuratibu na mwisho kutekeleza tukio hili hatakuwa salama, tutamsaka usiku na mchana hatimaye sheria itachukua mkondo wake," alisema Kamanda Sabas.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala, aliagiza Jeshi la Polisi kufanya operesheni hata kwenye mitandao ya kijamii kuwasaka wanaotoa ujumbe ambao unaleta uchochezi kuhusu sakata la Loliondo ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mangwala alisema kumekuwa na upotoshaji mkubwa unaofanywa na baadhi ya watu kwenye mitandao ya kijamii ambao wana agenda yao ya siri tofauti na uhalisia wa hali ilivyo.

"Wanaorusha picha, wanao-'comment negative' kulingana na mazingira na utofauti na uhalisia watafutwe popote kwa kutumia mifumo yoyote ile ili wachukuliwe hatua," alisema.

Tangu zoezi la kuweka mipaka katika pori tengefu la Loliondo lilipoanza wiki iliyopita, viongozi wamekuwa wakitoa onyo kwa baadhi ya watu wanaopotosha.

Miongoni mwa waliotoa onyo ni pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, ambaye alisema baadhi ya watu wanapotosha makusudi zoezi la uwekaji mipaka katika pori hilo kwa kuhusisha na suala la mgogoro wa wafugaji waliopo eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).



Naibu Katibu Mkuu - Uchukuzi, Dk. Ally Possi (kushoto), akiwa na makatibu wa wizara zinazosimamia uchukuzi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Burundi wakisaini ripoti ya wataalamu ya mradi wa reli ya kisasa ya SGR ya Uvinza-Musongati-Gitega-Bujumbura-Uvinza-Kindu wenye jumla ya kilomita 939, mjini Kinshasa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## BRELA yaziita kampuni zenye migogoro

**Na Halfani Chusi**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa siku saba kwa kampuni zenye migogoro kufikisha malalamiko yao kwao ili kutafutiwa ufumbuzi.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kampuni na Majina ya Biashara BRELA, Meinrad Rweyemamu, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kampuni nyingi kukabiliwa na migogoro.

Rweyemamu alisema kama zikiwa vizuri na migogoro ikatatuliwa ni rahisi kulipa kodi ya serikali, kujiendesha vizuri, kuleta mapato ya kila mwaka na kuongeza ajira kwa vijana.

"Kwa sasa tumekuja na kampeni hii yenye kaulimbiu inayosema 'Suluhisha na BRELA' baada ya kubaini ndani ya kampuni nyingi kuna migogoro mingi ambayo imesababisha baadhi kushindwa kujiendesha, hivyo tunaziomba kampuni zenye migogoro ya aina hiyo kufika katika viunga hivi vya Makumbusho Posta kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi," alisema Rweyemamu na kuongeza:

"Sisi BRELA, sio kwamba hatusikilizagi migogoro ya kampuni ila tumeona tutenge wiki maalumu kwa ajili ya kushughulikia migogoro, kwa hiyo nawasihi wamiliki wa hizo kampuni wafike kuanzia kesho (leo) saa tatu asubuhi hadi saa 11 jioni. Tutafanya kazi kwa saa 24 kwa ajili ya kushughulikia matatizo yao."

Rweyemamu alisema: "Hii kampeni sio kwa ajili ya hapa Tanzania pekee, hata kwa kampuni zilizopo nje ya nchi pia tunazishughulikia, lakini hata kwa walio mikoani kama wataweza kufika wafike, lakini tutaenda kuwatembelea huko huko lengo ni kuwasikiliza na kutatua migogoro."

Alitaja vikwazo kadhaa vilivyoko katika baadhi ya kampuni ikiwamo waendesha kampuni kutokuwa na elimu ya kutosha na kutojua sheria ya uendeshaji.

"Kwa mfano kwa mujibu wa sheria, lazima kampuni ilete kwa msajili wa kampuni taarifa yake ya mwaka. Ile fomu namba 128, lakini kampuni nyingi zikishasajiliwa zinasahau kupeleka taarifa mwisho wa mwaka kwa hiyo tunawashauri wafanyabiashara kupeleka taarifa zao."

# Shahidi aangua kilio akimtambua muuaji wa mumewe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, jana iliahirishwa kwa muda baada ya kusikiliza ushahidi uliotolewa na mke wa marehemu, Samwel Songoma, aliyeuawa kwa kupigwa risasi na majambazi waliopora fedha zake.

Shahidi huyo ambaye ni wa nne kwa upande wa mashtaka, alitolewa nje ya mahakama kwa muda baada ya kuangua kilio alipotakiwa kumtambua mtu aliyemuua mume wake.

Mshtakiwa katika kesi hiyo ni Daniani Adrea, maarufu Kamkono.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Jaji Lilian Itemba na alisomewa shtaka lake alikana kuhusika na kosa la mauaji ya Samwel Songoma kwa kumpiga risasi tumboni.

Upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Janeth Kisibo, ambaye alisema atakuwa na mashahidi watatu na yuko tayari kuwasikiliza.

Jaji Itemba alimuuliza wakili wa kujitegemea Penina Mashimba, anayemtetea mshtakiwa huyo kama yuko tayari kusikiliza mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri na kujibu yuko tayari.

Shahidi wanne wa upande wa Jamhuri, Elena Hemillana (46), ambaye ni mke wa marehemu, akiongozwa na Wakili wa Serikali Janeth Kisibo, alidai kuwa mwaka 2011 alikuwa anaishi katika Kijiji cha Lyobaika, Wilaya ya Bukombe na mume wake Samwel Songoma, ambaye kwa sasa ni marehemu aliyekuwa akifanya kazi ya kuuza madini.

Hemillana alidai Julai 2, mwaka 2013, majira ya usiku alikuwa nyumbani kwake wakiwa wamelala na mume wake na kuvamiwa na majambazi yaliyovunja mlango na kuingia ndani. Alidai kuwa majambazi hao waliomba fedha kwa mume wake na aliwapatia hizo, hata hivyo, hakuweza kujua jumla ya kiasi alichowapa.

Aliendelea kudai kuwa baada ya kuwapatia fedha hizo, majambazi hao walimwambia mume wake aongeze fedha, lakini aliwajibu kuwa hana zingine ndipo walipompiga risasi tumboni na kuanguka chini na kufariki dunia.

Shahidi huyo alidai kuwa majambazi hao waliingia chumbani na kuanza kutafuta fedha kwa kupekua vitu mbalimbali na kwamba wakati wakipekua alifanikiwa kumtambua mmoja wa majambazi hao.

Alimtaja kwa jina maarufu la Kamkono kwa sababu alikuwa fundi ujenzi katika kijiji hicho. Alipotakiwa na Wakili wa Serikali akaonyeshe mtu aliyemfahamu wakati wa tukio mahakamani hapo, shahidi huyo alimgusa bega mshtakiwa huyo na kuangua kilio akisema; "Ee Mungu wangu nisaidie, ee Mungu wangu nitie nguvu".

Shahidi huyo alitolewa nje ya mahakama huku akiangua kilio na baada ya nusu saa alirudishwa kizimbani na kuendelea kutoa ushahidi wake.

Mahojiano kati ya wakili na shahidi yaliendelea kama ifuatavyo:

**Wakili:** Utaratibu ulifanyika wa gwaride la utambuzi?

**Shahidi:** Hapana.

**Wakili:** Ganda la risasi liliokotwa wapi?

**Shahidi:** Nje.

Baada ya mahojiano hayo, wakili wa serikali aliomba mahakama hiyo iahirishe kesi hiyo hadi muda wa saa tisa jioni (**jana**).

Jaji Itemba alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi muda huo.

Awali, akisoma hati ya mashtaka, Karani wa mahakama hiyo Paschal Alphonce, alidai kuwa Julai 2, mwaka 2013, majira ya usiku katika Kijiji cha Lyobaika, Wilaya ya Bukombe, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimuua Samwel Songoma kwa kumpiga risasi tumboni na kufariki dunia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusikilize bajeti, tutoe maoni kwa wawakilishi wetu

**LEO** bajeti ya serikali ya kwanza tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani Machi 2021, inasomwa ambayo itaonyesha mwelekeo wa mwaka wa fedha 2022/23 kwenye mapato, matumizi na miradi ya maendeleo.

Wananchi watajielekeza jijini Dodoma kusikiliza wapi kutapunguzwa kodi, kutaongezwa au vyanzo vipya ambavyo vitaleta ahueni ya maisha kwa wananchi, hasa baada ya bidhaa nyingi kupaa bei kutokana na mafuta kupanda.

Bajeti hiyo ndiyo inabeba mwelekeo wa nchi katika kukusanya na kutumia kwenye matumizi ya kawaida, mishahara na miradi ya maendeleo ambayo inagusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Kubwa linalosubiriwa ni kusikia nafuu ya maisha kupitia kuondolewa kodi mbalimbali, ambazo kimsingi zimechangia bei ya mafuta kuzidi kupaa, na tayari Rais Samia, aliahidi hatua zaidi za kikodi zitatangazwa kwenye bajeti ya leo.

Mwezi uliopita mafuta yalishuka kidogo baada ya serikali kuingiza Sh. bilioni 100, ambazo zilileta nafuu ambayo bado haikusaidia bidhaa kushuka bei jambo ambalo wananchi waliona halijawagusa moja kwa moja.

Kwa miaka mingi bajeti imekuwa ikitegemea vyanzo vya mapato vya vinywaji baridi na moto ambavyo vimekuwa vikipanda, magari yanayoagizwa kutoka nje kiasi cha wabunge na wataalamu kuitaka serikali kuja na ubunifu kwenye eneo hilo.

Ipo ripoti ya Chenge One iliyopendekeza vyanzo vipya vya mapato, ikiwamo kuweka kodi kwenye uvuvi bahari kuu, lakini kutokana na gharama za uwekezaji bado nchi haijanufaika ipasavyo na vyanzo hivyo.

Kiu ya wananchi ni kusikia kama ni kicheko au maumivu zaidi kutokana na kuongezeka kwa kodi kwenye bidhaa mbalimbali, namna gani bidhaa za ndani zinalindwa, ili kuvutia zaidi wazalishaji na uwekezaji.

Lakini kuona miradi ya kimkakati kama bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere, reli ya mwendokasi (SGR) itakamilika, lakini ujenzi wa miundombinu mingine ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Bajeti hii itakwenda kuonyesha namna keki ya taifa itakusanywa na kugawanywa kwa usawa kwa Watanzania wote, ili kila mmoja ajisikie ni sehemu ya nchi kupitia miradi ya maendeleo na huduma za kijamii ambazo zinagusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Lakini kodi anayolipa inakwenda kwenye mfumo sahihi na inarudi kwake kupitia ujenzi wa huduma za kijamii kama shule, hospitali, zahanati, miundombinu na maji ambayo ni vya msingi kwa kila mmoja.

Ni muhimu Watanzania wakaisikiliza bajeti hiyo kwa kina itakaposomwa saa 10 kamili alasiri, ili kujua serikali imejipangaje na kodi zimeongezeka wapi.

Wapate pia nafasi ya kuwashauri wawakilishi wao katika muhimili huo nini cha kuchangia wakati wa kuchambua bajeti hiyo kwa siku tano, ili wanaposimama wawe na la kuzungumza.

Pia ni vizuri wabunge wakawataka wananchi wa majimbo yao kusikiliza bajeti na kuwasiliana na wachache, ili kuwashauri ni hoja gani wazichambue kwa maslahi mapana ya wananchi wa jimbo na taifa kwa ujumla.

Naamini wabunge wana makundi ya mtandaoni ya wananchi wao, ni muhimu kuwahamasisha kusikiliza bajeti na kutoa maoni yao ili kwa siku mbili wanazopewa wabunge hao kwa ajili ya kutafakari kupata hoja za kuchangia ambazo zitasaidia maboresho ya bajeti.

Bajeti kikomo ya mwaka huu ni Sh. trilioni 41.063 kwa mwaka 2022/23, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.1 ikilinganishwa na bajeti ya Sh. trilioni 37.980 mwaka 2021/2022.

Kati ya fedha hiyo Sh. trilioni 25.542 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni asilimia 62.2 ya bajeti yote, ikiwa ni Sh. trilioni 11.308 kwa ajili ya ulipaji deni la serikali na gharama nyingine.

Aidha, matumizi ya maendeleo yanatarajiwa kuwa Sh. trilioni 15.521 sawa na asilimia 37.8 ya fedha yote, kati yake Sh. trilioni 12.22 fedha za ndani na Sh. trilioni 3.399 ni fedha za nje.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Lydia Sospeter, TUDARCO

# Hili la wanaume kufa na tai shingoni, hapana

**KUMEKUWA** na matukio mengi kwenye jamii mijini na vijijini yanayohusisha wanaume kufanya maamuzi kwa sababu ya kukaa na vitu moyoni.

Matokeo yake wanajikuta wakitumbukia katika maamuzi magumu na ya kikatili kama mauaji ya wenzao wao au wenyewe kujitia kitanzi.

Huenda wengi wamekuwa wakidhani ni udhaifu kusema matatizo yao binafsi na yale yanayowahusisha wenza wao na hapo ndipo kesi za mauaji zinapoleta simanzi kwenye mioyo yao na Watanzania wengine.

Matokeo yake hawatafuti ushauri na nasaha na kama wanavyosema mwanzo wa ngoma ni lee, mauaji haya yalianza kama kipele ila sasa ni jipu linalohitajika kutumbuliwa kwa upasuaji mkubwa.

Katika siku za hivi karibuni, ripoti na taarifa kuhusu kuenea kwa vitendo vya mauaji yanayohusishwa na wivu wa kimapenzi vimezua taharuki, mjadala pia hofu.

Siku za nyuma hayakusikika sana matukio hayo, ila kwa sasa yameonekana kushamiri. Swali la kujiuliza ni hili ni kwanini mauaji haya? Je, nini kinachoendelea kwenye jamii?

Kumekuwa na matukio ya kujiua, wanawake na wanaume wakijinyonga, lakini wanaume kuua wake na wapenzi wao, lakini kinamama kuua waume zao, kisa hisia za kuwapo harufu ya usaliti kwenye uhusiano au ndoa inaponukia.

Hili huenda linatokana na wanaume kushindwa kuongea matatizo yao kwa wanasihi au watu wa karibu ama wataalamu wa saikolojia kwa kuogopa aibu.

Ni kwa sababu wanaume ndiyo wanadaiwa zaidi kuhusika na mauaji hayo.

Kumekuwa na mifano kadhaa wa kadhaa, ya vitendo hivi mfano jijini Mwanza hivi karibuni mke na mume walikufa kwa risasi.

Tukio hili ni kama limeibua upya mjadala wa masuala ya mauaji kutokana na madai ya kuwapo wivu wa mapenzi.

> **Mpe uhuru mwenzio aishi maisha ayapendayo lakini heshimuni na kulinda mambo mliyokubaliana ili kuepuka mafarakano.**

Tukio lingine ni la Februari 24, mwaka huu, huko Mwanga, Kilimanjaro lilihusisha wanaume wawili waliokuwa na uhusiano na mwanamke mmoja, kuamua kula njama na kumuua kwa sababu ya wivu na aibu ya kuwachanganya kimapenzi.

Kabla ya kumuua kwa kumkatakata kwa mapanga kuna madai kuwa walimbaka na kumdhalilisha. Lakini pia tukio lingine ni la Desemba 27, 2021 mwalimu wa sekondari mkoani Singida, alidaiwa kuuawa kwa kuchomwa moto na mkewe baada ya kumtuhumu kuwa na uhusiano na mwanamke mwingine.

Oktoba mwaka jana katika kitongoji cha Kanyabugulu mkoani Kagera, mwanaume alidaiwa kumuua mkewe kwa kumkata mapanga nyumbani kwake akishuhudiwa na mtoto wake wa miaka 14, kwa kile alichodai mwanamke huyo alikuwa na uhusiano na mwanaume mwingine.

Ukitazama kwa undani vitendo hivi vya mauaji ni suala la kisaikolojia zaidi, maana mtu anakuwa na imani kwamba akimuua mwenzake atafaidika. Kuua hakufanyiki kwa ghafla ni mtiririko wa matukio yanayoenda kupanga hadi kuamua mauaji.

Hivyo basi ili kuepukana na haya yote ni vyema kama wapenzi wakikaa na kutengeneza namna yao ya kuishi, wakubaliane walivyo na madhaifu yao na kukubaliana yale ambayo wanatofautiana.

Mpe uhuru mwenzio aishi maisha ayapendayo lakini heshimuni na kulinda mambo mliyokubaliana ili kuepuka mafarakano.

Na pia serikali iweke adhabu kali zaidi kwa watu watakaojihusisha na vitendo hivi maana isipoziba ufa itajenga ukuta.

Sio hivyo tu lakini ni vyema kuondokana na dhana inayowafanya wanaume wajione wadhaifu mbele ya jamii iwapo watasema matatizo wanayopitia hasa katika mapenzi wataweza kupata msaada wa afya ya kiakili na kuzuia maafa mengine.

Kutoa dukuduku au kufunguka kuhusu matatizo inasaidia kuachia mzigo uliobeba moyoni na huleta afya na faraja ya akili, moyo na mwili.

## DCB yajivunia mikopo ya trilioni moja miaka 20

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya DCB inasherehekea miaka 20 tangu kuanzishwa kwake ikijivunia kutoa mikopo ya zaidi ya Sh. trilioni moja, wateja zaidi ya 200,000 na kutoa huduma bora zinazokidhi mahitaji ya kifedha ya wateja wao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa DCB, Godfrey Ndalahwa, alisema katika miongo miwili ya mafanikio, benki hiyo imeshuhudia ikipiga hatua mbalimbali za maendeleo, kutokana na uongozi bora uliopo.

"Miaka 20 ya mafanikio ya DCB, benki yetu imekuwa mstari wa mbele kutoa fursa mbalimbali za kiuchumi kwa Watanzania wenye vipato tofauti, kwa wajasiriamali wadogo, wakati na wafanyabiashara wakubwa. Tunashirikiana na serikali katika juhudi za kusaidia wananchi kiuchumi," alisema.

Alisema kwa miaka 20 wamebuni na kuingiza bidhaa mbalimbali zenye ubunifu wa hali ya juu zikiwamo huduma za kibenki kwa njia za kidigitali kwa malengo ya kusogeza huduma bora za DCB karibu na wateja na huku ikiunganishwa na mfumo wa malipo ya serikali (GePG) unaowezesha wateja wao kulipa maduhuli ya serikali kwa urahisi kupitia matawi na mifumo ya mtandaoni.

"Katika kuonyesha kuwa DCB inajali maisha ya Watanzania tulianzisha akaunti ya elimu ya DCB Skonga inayomsaidia mzazi kuwekeza na kuwa na uhakika kwa ajili ya elimu ya mtoto wake hadi chuo kikuu, lakini pia tuliboresha zaidi dirisha letu huduma za kidigitali kwa kuongeza huduma zaidi zikiwamo DCB Kibubu inayomwezesha mteja kujiwekea akiba, lakini DCB Kidigitali," alisema mkurugenzi huyo.

"Benki inatarajia kufungua matawi mapya matano na vituo vidogo (DCB Jirani) vipatavyo 28 kwa sasa benki ina matawi tisa likiwamo tawi letu la Dodoma na tawi jipya la Victoria," alisema Ndalahwa.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa DCB, Zawadia Nanyaro, alisema benki yao ilianzishwa mwaka 2002 kama ya kijamii kutokana na kilio cha wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam kukosa huduma za kifedha hasa mikopo kwa wajasiriamali wadogo hasa wanawake ikiwa na mtaji wa Sh. bilioni 1.7.

Alisema mtaji huo ulitokana na wanahisa waanzilishi watano ambao ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manisapaa za Temeke, Kinondoni na Ilala pamoja na wananchi waliojitokeza kununua hisa.

Alisema mtaji umefikia Sh. bilioni 30 na kuiwezesha kukidhi masharti ya Benki Kuu (BoT) ya kujiendesha kama benki ya biashara na kuiongezea uwezo mkubwa wa kushindana katika soko.

Pia wamefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni moja ulionufaisha watu 400,000 tangu kuanzishwa.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa kwanza wa DCB, Edmund Mkwawa, alisema; "tulianza na kuhudumia hasa wafanyabiashara wadogo na wanajeshi, lakini huduma za benki hii zilikuwa zikipanua siku hadi siku na kufungua matawi mpaka mikoani na vituo vidogo vya kutoa huduma za kibenki nimefurahi sana kuyaona mafanikio haya adimu."

# RC atoa saa 24 kupata majina wanaokwamisha miradi

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, ametoa saa 24 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, Geofrey Nnauye, kuwasilisha majina ya watumishi na wakuu wa idara ambao wamekuwa kikwazo cha kutokukamilika kwa miradi ya maendeleo wilayani humo.

Akitoa agizo hilo, Mgumba alisema baadhi ya watumishi wasio waadilifu wamekuwa wakimchonganisha Rais Samia na wananchi kwa kutokamilisha miradi ya maendeleo.

Mgumba alitoa agizo hilo baada ya wajumbe ambao waliambatana naye katika ukaguzi wa miradi hiyo kuibua hoja ya uzembe unaofanyika katika baadhi ya miradi wilayani Ileje.

Baada ya kauli kutoka kwa wajumbe hao ndipo Mgumba alipotaka kupata majibu na sababu ya miradi mbalimbali ya maendeleo kukwama wakati serikali imetoa fedha.

Hata hivyo, hakupata majibu sahihi na kumtaka Mkurugenzi Mnauye kumkabidhi majina ya wahusika ndani saa 24 ili awashughulikie.

"Mnataka kunichonganisha na Rais Samia Suluhu Hassan. Fedha nyingi zimekuja za ujenzi wa miradi halafu ujenzi unasuasua ili mimi nitumbuliwe, sasa kabla ya mimi kutumbuliwa naanza na ninyi."

Mkazi wa Kijiji cha Shinji, Faridi Mkumbwa, alisema wilaya hiyo ipo pembezoni mwa Mkoa wa Songwe na ni mpakani mwa nchi ya Malawi, lakini maisha wanayoishi ni kama wamesuswa.

Alisema wilaya yao imekuwa ya mwisho kwa ufaulu shuleni, ya mwisho kwenye ukusanyaji mapato pia ni ya mwisho katika ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Mkazi mwingine wa Ileje, Hassan Mwampashe, alisema tatizo kubwa lililoko kwa wilaya hiyo ni watumishi kukaa muda mrefu katika kituo cha kazi na kujenga mazoea ya kiutendaji.

Aliishauri serikali kuweka utaratibu wa kuwahamisha watumishi kila baada ya miaka miwili ama mmoja ili kujenga nidhamu ya kazi.

"Hebu angalia serikali imetoa fedha nyingi kujenga miradi ya maendeleo katika idara zote, lakini hakuna mradi unaokamilika kwa wakati huku mapungufu yakiwa lukuki, ni bora wakuu wa idara husika wahamishwe kujenga nidhamu ya utendaji kazi."



Mbunge na Balozi wa Kodi wa Hiari wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Subira Mgalu (kulia), akisubiri kupatiwa risiti ya kodi ya kielektroniki ya EFD baada ya kununua bidhaa katika duka la mfanyabiashara wa Soko la Mjimwema Mafinga wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi wilayani Mufindi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UNESCO yaombwa kusaidia vita ukatili wa kijinsia nchini

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, ametoa wito kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kusaidia kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto nchini.

Dk. Gwajima alitoa wito huo juzi, jijini Dar es Salaam alipokutana na wajumbe kutoka UNESCO wakiongozwa na Kaimu Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo, Faith Shayo.

Alisema shirika hilo limeisaidia serikali kukabiliana na ukatili wa kijinsia kupitia mkakati wa kitaifa ulioanzishwa mwaka 2017 na kumalizika Juni, mwaka huu.

"Kupitia mkakati huo UNESCO imefanya kazi kubwa, pia tunatarajia itashiriki katika mkakati ujao wa miaka mitano wenye lengo la kupaza sauti kupinga ukatili," alisema na kuongeza:

"Wakati tunajiandaa kwa Siku ya Mtoto wa Afrika na mkakati mpya hali ya sasa inahitaji ushirikiano wa dhati wa wadau wote ili kurejesha usalama kwa wanawake na watoto," alisema.

Aliongeza kuwa ukatili kwenye hali ya ulawiti na ubakaji umezidi, jamii inahitaji kupaza sauti kupinga hali hiyo huku akitoa wito kwa wanaume wenye nia njema kuunda jukwaa la kukemea vitendo vinavyotokea sasa.

Aidha, alibainisha kwamba anatambua UNESCO ina miundombinu ya kutosha hasa redio ambazo zinawafikia wananchi kwa kulingana na maeneo, huku akiwataka kuitumia kupinga ukatili na kwamba serikali ingependa kutumia mifumo ya kupasha habari ya shirika hilo kuendesha kampeni kubwa ya kupinga ukatili.

Kaimu Mwakilishi Mkazi wa Shirika hilo, Faith Shayo, alisema UNESCO ipo tayari kushirikiana na serikali kuinua ustawi wa jamii kupitia kuboreka kwa mahusiano ya kijinsia na kuondoa ukatili.

Pia, aliipongeza juhudi za kampeni ya mlango kwa mlango iliyoanzishwa na wizara husika kukabiliana na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

"Pamoja na kwamba tunaendelea kushirikiana na serikali katika kutoa elimu ya afya na huduma za jamii kupitia miradi yetu katika vyuo nchini na nchi za Jumuiya ya SADC ili kutengeneza makazi salama, UNESCO pia ipo tayari kuingia makubaliano na serikali juu ya namna bora ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia," alisema Waziri Gwajima.

Vile vile, alitaja baadhi ya miradi ambayo UNESCO inaendelea kushirikiana na serikali ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wafanyakazi na viongozi kuhusu ukatili wa kijinsia unavyokuwa na namna ya kukabiliana nao na kuwezesha kuwapo kwa mada maalumu zinazozungumzia ukatili huo.

# Maofisa kilimo wapewa angalizo matumizi pikipiki

**Na Happy Severine,**
BARIADI

MAOFISA kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu wamepewa angalizo juu ya matumizi sahihi ya pikipiki walizopewa ili kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Pia, wametakiwa kutozitumia katika matumizi binafsi ya starehe.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Adrean Jungu, wakati akikabidhi pikipiki nane kwa watendaji hao.

Alisema Wizara ya Kilimo imetoa pikipiki hizo ili kuwawezesha maofisa kilimo kufika katika maeneo ambayo hapo awali walikuwa hayafikiki na kuwasaidia wakulima kulima kilimo bora na chenye tija.

"Leo tunagawa pikipiki nane kwa maofisa kilimo wanane wa Halmashauri ya Mji ili kuwawezesha kufika maeneo ambayo yalikuwa hayafikiki... vyombo hivi ni vya thamani na vyenye gharama kubwa, hivyo ni wajibu wa kila ofisa kuvitunza na msije kuonekana mnazitumia kwa matumizi mengine tofauti na yaliyokusudiwa," alisema Jungu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, David Masanja, alisema Wizara ya Kilimo imefanya jambo kubwa na muhimu kuboresha na kuleta tija kwenye kilimo.

Masanja alisema anaamini kuwa pikipiki hizo endapo zitatumika kwa mlengo uliokusudiwa zitaongeza tija na kasi ya uzalishaji wa mazao.

"Watendaji wakuu tujitahidi sana kutunza vyombo hivi... tutumie kwa mlengo uliokusudiwa ili kuongeza tija katika uzalishaji...mwaka jana kwenye pamba tulivuna tani 5,000 na kwa sasa tumepata vitendea kazi, hivyo uzalishaji uongezeke zaidi ya hapo," alisema Masanja.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Bariadi, Issa Mtweve, alisema wanaishukuru serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuona na kutambua umuhimu wa kukifanya kilimo kiwe na tija kwa kutoa vitendea kazi hivyo.

Mtweve alisema kupitia pikipiki hizo walizopokea matarajio yao ni kuwafikia wakulima 17,000 ambao hapo awali ilikuwa ni ngumu kuwafikia wote.

Ofisa Kilimo Kata ya Mhango, Samweli Paul, alisema pikipiki hizo zitawasaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wao na kuhakikisha wanawafikia wakulima wote na kuwapatia elimu husika ya kilimo bora na chenye tija.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, akifunga mkutano wa wadau wa masuala ya mbegu nchini, uliolenga kujadili hali ya sekta ya mbegu na matumizi ya mbegu bora, uliofanyika kituo cha utafiti wa mboga na matunda cha kimataifa cha World Vegetables Center. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAF Mvomero yawajengea uwezo wawezeshaji

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro imewajengea uwezo wawezeshaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) ili walengwa wa mpango huo katika vijiji 130 wanufaike zaidi.

Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF wilayani humo, Mweta Khalid, alisema lengo ni kuwajenga uwezo wawezeshaji hao zaidi ya 100, ili nao wakatoe elimu kwa walengwa namna bora ya kutumia fedha hizo.

Alisema wawezeshaji hao pia wamejengewa uwezo ili wakawawezeshe walengwa kutumia fursa ya vikundi vyao ambayo tayari vimeshaundwa kwa ajili ya kujiongezea kipato kupitia mpango wa uweka akiba na kukuza uchumi wa kaya.

Alisema walengwa wanatakiwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa ushiriki wao ni moja ya njia ya kujiongezea kipato cha kujikimu kimaisha.

Kwa upande wake Mratibu wa TASAF awamu ya tatu katika wilaya hiyo, Mahija Mdoe, alisema mafunzo yametolewa kwa muda wa siku tatu kwa wawezeshaji juu ya uhaulishaji wa fedha kwa walengwa.

Alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo mzuri wawezeshaji hao ngazi ya wilaya ili kuboresha warsha za jamii zinazofanyika wakati zoezi la malipo litapokuwa likifanyika kuimarisha zaidi shughuli zote za mpango huo.

"Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wawezeshaji hawa wa ngazi ya wilaya ili kuboresha warsha za kijamii kabla ya malipo kwani kabla ya zoezi hilo la malipo kufanyika ni vizuri kukawa na warsha kwenye ngazi ya jamii," alisema.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema watahakikisha zoezi la utoaji ruzuku kwa walengwa linafanyika kikamilifu kwa wanaohusika na mpango na lengo ni kuona fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya zoezi hilo zinawanufaisha walengwa.

Justine Munyombe ni miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo alisema amejifunza namna ya uhaulishaji wa fedha kwa walengwa vijijini na kuahidi kusimamia zoezi kikamilifu pamoja na kutoa elimu kwa wahusika wa mpango huo.

## WFP yawapiga msasa wakulima maharagwe, mahindi

**Na Faustine Feliciane,** KIGOMA

WAKULIMA wa mahindi na maharagwe Wilaya ya Kasulu, mkoani hapo, wamepewa elimu ya soko la uhakika la mazao yao kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

WFP wametoa elimu hiyo katika nyanja za uandaaji shamba, uvunaji na utunzaji wa mazao, pia wakinunua mazao hayo kwa wakulima kwa ajili ya kulisha kambi za wakimbizi.

Akizungumza na waandishi wa habari wilayani Kasulu, Mkuu wa WFP Wilaya ya Kasulu, Michael Bisama, alisema WFP kwa kuungana na mashirika mengine ya UN wanatekeleza mradi wa pamoja wa Kigoma (Kigoma joint program-KJP), ukiwa na lengo la kuwaimarisha wakulima wadogo na kuwainua kiuchumi.

"Baada ya kutoa elimu tangu kuanza kwa mradi huu mwaka 2018, wakulima wameongeza mazao wanayovuna, WFP tumekuwa wanaunuzi wakubwa wa mazao yao japo kiukweli bado hayajifikia idadi ya tani tunazozitaka.

"Lakini taratibu wameanza kuzalisha mazao mengi ukilinganisha na namna walivyokuwa wanavuna kabla ya kupata elimu," alisema Bisama.

Alisema kwa mwaka 2020, WFP ilihitaji tani 2,000 za mahindi, lakini walipata tani 300 pekee walizonunua kwa wakulima hao.

"WFP tunahudumia kambi za wakimbizi, kwa mwezi tunahitaji tani 1,000 kwa ajili ya Kambi ya Nyalugusu ambayo ina wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Burundi, tunashukuru kwa sasa uzalishaji kutoka kwa wakulima unaongezeka, mfano kwa mwaka jana tulinunua tani zaidi ya 1,300, hii imetokana na wakulima kufuata kilimo cha kisasa na kufanikiwa kuongeza uzalishaji," alisema Bisama. Alisema WFP imekuwa ikinunua maharagwe kwa bei nzuri inayowapa tija wakulima na kubadilisha bei za mazao kutoka kwa wanunuaji wengine.

"Huko nyuma wakulima walikuwa wanauza maharagwe kwa hela ya chini kuanzia Sh.1,000 na ilikuwa haivuki Sh. 1,400, lakini sisi baada ya kutoa elimu na wakulima kuzalisha mazao yenye viwango tulinunua kwa Sh. 1,950 na kuwafanya wanaunuzi wengine kuuza kwa bei hiyo na wakulima walinufaika sana," alisema Bisama.

Mmoja wa wakulima waliopata elimu hiyo, Milambo Masoud, kutoka Kijiji cha Nyumbigwa, alisema ujio wa WFP kuwekeza kwenye kilimo wilayani humo kumesaidia uzalishaji wenye tija na kuinua vipato vya wakulima.

Mkulima mwingine kwenye kata hiyo, Zipora Mussa, alisema kupitia mradi huo, WFP wametoa mashine za kupukuchulia mahindi na kumpunguzia mkulima kazi ya kupiga mahindi.

## SBL kuwasaidia vijana kushiriki kwenye kilimo

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL), imesema itaendelea kusaidia kutengeneza mazingira wezeshi kwa vijana kushiriki kwenye sekta ya kilimo kwa manufaa ya uchumi wa nchi.

Hayo yalibainishwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Uhusinao kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, kueleza kuwa Tanzania ina idadi kubwa ya vijana ambao wanaweza kutoa mchango kwenye sekta ya kilimo.

"Kilimo ni moja ya sekta yenye mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Nchi yetu pia ina idadi kubwa ya vijana ambayo ni nguvu kazi. SBL tunatambua umuhimu wa vijana kushiriki kwenye kilimo na tupo mstari wa mbele kuhakikisha ushiriki wao unakuwa mkubwa zaidi," alisema Wanyancha.

Wanyancha alisema SBL kupitia programu yake ya kilimo viwanda imekuwa ikitoa ufadhili wa masomo kwa vijana wanaosomea fani za kilimo, lengo likiwa ni kusaidia kuongeza wataalamu vijana kwenye kilimo.

"Kupitia programu ya kilimo viwanda tunalipia gharama zote na kwa kipindi chote cha masomo ambacho vijana wanufaika wanakuwa masomoni. Katika programu hii pia tunatoa nafasi za vijana kujifunza kwa vitendo," alisema Wanyancha.

Alisema kupitia programu hiyo SBL tayari imeshatoa ufadhili kwa wanafunzi zaidi ya 200 wanaosomea masomo ya kilimo katika vyuo vinne vya Kaole cha Bagamoyo, Kilacha cha Moshi Mt. Maria Goretti cha Iringa na Igabiro kilichoko Muleba, mkoani Kagera.

Mkurugenzi huyo alisema SBL pia ina programu nyingine ya kilimo biashara ambayo inafanya kazi na wakulima zaidi ya 400 ambao huzalisha malighafi za kutengenezea bia na kuiuzia kampuni hiyo.

Wanyancha alisema, mradi huo unawasaidia wakulima wanaolima mahindi, mtama na shayiri walioko katika sehemu mbalimbali nchini kupata soko la uhakika la mazao yao kwa kuwa kampuni hiyo hununua nafaka hizo kwa ajili ya viwanda vyake vya Moshi, Dar es Salaam na Mwanza.

"Mpaka sasa, wakulima 400 wananufaika kutokana na mradi huu. Tunawapatia mbegu bora bure, tunawaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya kupata mitaji ya kupanua uzalishaji wao na pia tunawapatia mbolea na pembejeo nyingine za kilimo," alisema.

# TTCL kuwalinda wateja wake mtandao wa simu

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL), kupitia T-PESA limezindua huduma ya Lipa kwa Uhakika kwa lengo la kumlinda muuzaji na mnunuzi kwa njia ya simu.

Akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa T-PESA, Lulu Mkudde, alisema huduma hiyo itakuwa ni suluhisho kwa makundi hayo, kwa kuwa itasaidia kuondoa udanganyifu.

Alisema, uzinduzi wa huduma hiyo umefanywa kwa kushirikiana na kampuni inayojishughulisha na masuala ya kijamii iitwayo NGASMAKE, inayowahakikishia wahusika usalama wa bidhaa zao.

"Mfumo huu utamhakikishia mnunuzi usalama wa fedha zake hadi atakopata bidhaa au huduma ambapo anaweza kurudisha malipo yake ikiwa bidhaa haijafikishwa kwake," alisema.

Vile vile, muuzaji atafaidika kwa uwapo wa mfumo huo, kwa kuwa atakuwa na uwezo wa kupokea taarifa ya malipo kabla hajatoa huduma, hali ambayo inampa uhakika wa malipo.

"Nitoe wito kwa wanunuzi wa huduma au bidhaa kupitia mitandao ya kibiashara inayopatikana nchini kutumia mfumo huu, kwani unatoa usalama wa fedha za wateja. Huduma hii inapatikana kwa kupiga menyu *150*71# kisha kuchagua namba 4 yenye Huduma ya Lipa Kwa Uhakika,"alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa NGASMAKE, Emmanuel Ngalya, alisema, kampuni hiyo inatoa huduma ya mfumo wa kifedha unaomlinda muuzaji na mnunuzi, ili kukabili changamoto za kiusalama katika biashara ya kimtandao.

"Miongoni mwa changamoto hizo ni utapeli na udanganyifu, nasi tumekuja na mfumo rafiki na salama wa Lipa kwa Uhakika, utakaosaidia kuondoa changamoto hizo na kupata bidhaa zenye viwango," alisema Ngalya.

Alifafanua kuwa kupitia mfumo huo, mnunuzi akishanunua bidhaa na kulipia T-PESA, fedha hazitaenda moja kwa moja kwa muuzaji, zitahifadhiwa kwenye mfumo hadi atakopapata bidhaa yake na kuthibitisha kama ndiyo aliyoagiza na ndipo unaruhusu fedha kwenda kwa muuzaji.

"Mfumo huu umewekwa vizuri kwa watumiaji, endapo watapata changamoto yoyote, aidha ya kukosa huduma, watapiga namba maalum ya kituo cha huduma kwa wateja 0800110137 au kurasa za mitandao ya kijamii," alisema.




Ofisa Rasilimali Watu Mwandamizi wa Barrick North Mara, Daniel Paul, akiwagawia wanafunzi zawadi ya flash wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustine, Mwanza, katika kongamano la kuwajengea uwezo lililotayarishwa na Taasisi ya AIESEC na kudhaminiwa na Barrick lililofanyika chuoni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# IJC yatakiwa kuandaa mpango utendaji kazi

**Na Mary Gwera**

MSAJILI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Wilbert Chuma, amewataka watumishi wa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki (IJC) Kinondoni, kuandaa mpango wa kutekeleza utendaji kazi utakaolenga kumridhisha mteja kulingana na huduma zinazotolewa na kituo hicho.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga mafunzo ya huduma kwa mteja.

Chuma alisema ana imani kuwa mafunzo waliyopata watumishi hao yatawasaidia kutokufanya kazi kwa desturi na mazoea ya awali bali kufanya kazi kwa weledi.

"Nina imani kuwa wananchi wanaokuja kupata huduma katika Mahakama Jumuishi wapate huduma zilizo bora, hivyo ni muhimu kuzingatia mafunzo haya kwa kuleta tija, na hayatakuwa na maana kama hamtayatekeleza kwa vitendo," alisema Chuma. Pia aliwataka watumishi hao kutekeleza maelekezo ya viongozi hususani matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), katika kusikiliza mashauri kwa njia ya runinga na maelekezo ya Jaji Mkuu kupitia kaulimbiu ya 'Zama za mapinduzi ya nne ya viwanda: Safari ya maboresho kuelekeza mahakama mtandao na kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa'.

"Kufanyika kwa mafunzo haya kutakuwa chachu ya kuboresha huduma zitakazotolewa na Mahakama pamoja na wadau wake ili kuleta maana halisi ya uanzishwaji wake," alisema.

Mafunzo hayo ya siku tano ambayo pia yalifanyika katika Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki (IJC) Temeke, yalihudhuriwa na watumishi wote wa vituo hivyo pamoja na wadau wa Mahakama.

Katika mafunzo hayo, mada zilizotolewa ni pamoja na utoaji wa huduma ya kwanza, maadili ya msingi na utamaduni wa Mahakama.

Zingine ni mkataba wa huduma kwa mteja, maadili yaliyobinafsishwa ndani ya Mahakama ya Tanzania, usawa katika taaluma na mwonekano wa mtu, masuala ya kisaikolojia kanuni za maadili yanayofaa na huduma kwa mteja kuendana na viwango vya IJC.

# Serikali kukamilisha maboma 300 ya zahanati

BUNGE limeelezwa kuwa katika mwaka ujao wa fedha 2022/23, serikali imetenga Sh. bilioni 15 kukamilisha maboma ya zahanati 300 kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Christina Mnzava.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema serikali imehamasisha wananchi kujenga zahanati kila kata na vijiji na maboma mengi hayajakamilika nini kauli ya serikali kukamilisha maboma hayo hasa kwa Halmashauri ya Shinyanga.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema serikali ilihamasisha wananchi kwa nia njema kuhakikisha wanapata zahanati na vituo vya afya katika maeneo ya kimkakati na mpango wa serikali ni kukamilisha zahanati na maboma ya vituo hivyo.

Alisema katika mwaka mmoja uliopita maboma ya zahanati 954 yamekamilishwa.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Mwibara (CCM), Charles Kajege, alihoji lini serikali itakamilisha majengo ya shule na zahanati ambayo yalijengwa kwa nguvu za wananchi katika Jimbo la Mwibara.

Akijibu swali hilo, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imepeleka Sh. milioni 287.5 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 24 katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 serikali imetenga Sh. milioni 240 kwa ajili ya kukamilisha vyumba vya madarasa 14 katika Jimbo la Mwibara pamoja na ukamilishaji wa maabara tatu za Kemia, Baiolojia na Fizikia.

"Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati, katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali imekwisha peleka kwenye Jimbo la Mwibara Sh. milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha maboma mawili ya zahanati za Sozia na Ragata," alisema.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2022/23 Sh. milioni 88, imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya Nyamitwebiri.




**Habari zote: Augusta Njoji , DODOMA**



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa (kushoto), akishauriana jambo na baadhi ya wabunge ndani ya ukumbi wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Songwe kujengewa chuo cha ufundi stadi

SERIKALI ipo mbioni kuanza utekelezaji wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma (VETA) cha Mkoa wa Songwe na tayari eneo lenye ukubwa wa ekari 50 limetengwa.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, alieleza hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA katika Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe ili kuwezesha vijana wa mkoa huo kupata maarifa na ujuzi na kuweza kujiajiri.

Akijibu swali hilo, Kipanga alisema chuo hicho kinatarajiwa kujengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 2.99 kupitia mapato ya ndani ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na ujenzi huo unatarajia kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Katika swali lake la nyongeza, alisema mahitaji ya chuo hicho ni ya muda mrefu na kuhoji lini zabuni za ujenzi zitatangazwa.

"Vijana wengi wa Songwe wanahitaji chuo na inawezekana ikachukua muda mrefu kukijenga, je, serikali ipo tayari kutumia majengo mbadala kutoa mafunzo hayo?" Alihoji.

Akijibu, alisema kwenye ujenzi kuna namna tofauti tofauti na kwamba itategemea njia itakayotumika kwenye ujenzi huo ingawa VETA imekuwa ikitumia 'force account'.

Alisema mwaka wa fedha utakapoanza Julai mosi, mwaka huu, mchakato wa ujenzi huo utaanza, kwa kuwa kwa sasa maandalizi yanaendelea ili eneo hilo lipate hati miliki.

"Kuhusu majengo mbadala baada ya mkutano huu wa bunge kuisha, nitafanya ziara na timu ya wataalamu ili kufanya tathmini ya hayo majengo yatakayotumika kwa kipindi kifupi wakati tukiendelea na ujenzi," alisema.

# Mbunge ataka polisi kukabiliana na vitendo vya ukatili kijinsia

KUTOKANA na kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa hivi karibuni, Mbunge wa Viti Maalum, Ester Bulaya, ametaka Jeshi la Polisi kuweka mikakati mahsusi ya kukabiliana na wimbi la vitendo hivyo nchini.

Akiuliza swali bungeni jana, alisema kwasasa kuna wimbi la ukatili kwa wanawake kuuliwa na watoto kufanyiwa vitendo vya ajabu.

"Bado hatujaona jitihada za dhati za serikali kupitia Jeshi la Polisi kukabiliana na uhalifu huu wa kuwadhuru wanawake na watoto ambao wanatakiwa kulelewa vizuri wawe watumishi bora huko baadaye," alisema.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, akijibu swali hilo, alikiri kuwa matukio mengi yanaripotiwa ya uhalifu unaohusisha mauaji na mateso kwa watoto.

Alisema ipo haja ya wazazi, walezi na viongozi wa dini kushirikiana kukomesha uhalifu huo na jeshi hilo limekuwa likichukua hatua bila kumchelea mtu pindi unapotokea uhalifu huo.

Aliahidi serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa amani kukabiliana na vitendo hivyo.

Katika swali lingine la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alisema kumezuka vikundi vya uhalifu katika Kata ya Makulu, Jiji la Dodoma vinavyojiita 'Panya Kalowa' na kutaka kujua nini mkakati wa serikali kuvidhibiti vikundi hivyo kwenye maeneo mengine.

Naibu Waziri Sagini, alisema tayari polisi Dodoma wameanza kudhibiti vikundi hivyo na kuna vijana wametiwa nguvuni tayari huku akilihakikishia Bunge kuwa watawashughulikia hao panya kalowa.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Pangawe (CCM), Haji Amour Haji, alihoji serikali ina mpango gani wa kukabiliana na matukio ya uhalifu ukiwamo wizi katika Jimbo la Pangawe.

Sagini alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi itaendelea na kazi ya kulinda maisha ya watu na mali zao, kwa kufanya doria, kuendesha operesheni mbalimbali na misako, ili kuwabaini na kuwakamata wahalifu.

Alisema Jeshi la Polisi limewapanga wakaguzi wa polisi kila shehia katika Jimbo la Pangawe ili kusimamia usalama na kuishirikisha jamii kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi.

INAPOTIMIZA UMRI MIAKA 56

## Jifunze; sura kamili ya BOT, ilikotoka, iliko na inakoelekea



Ukurasa 13

Nipashe

# TESA

Jumanne Juni 14, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 12

## Usafiri mabasi ya shule; huduma yenye hofu ya ajali, kuchoka, kukosa usingizi

ELIMU NA SABATO KASIKA

# Vita ya rushwa ya ngono shuleni

• Watoto watajua tambua 'fataki'

HADAA na kuwarubuni wanafunzi mabinti kingono ni kikwazo cha maendeleo yao kielimu kwa vile kunaweza kuleta mimba za utotoni, kukatisha masomo, kuambukizwa maradhi na kuvuruga hatima za wasichana wengi.

Ni tatizo linalopigiwa kelele na wadau wengi na jitihada mbalimbali zinazofanywa kusaidia wanafunzi kusoma hadi kuhitimu bila kukwamishwa na 'mafataki'.

Taasisi ya Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) ni miongoni mwa 'machampion' wa jitihada hizo.

Wamejikita kwenye baadhi ya shule za msingi na sekondari wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni Dar es Salaam.

Taasisi hiyo inafanya kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', kwa kushirikiana na wadau ikifundisha wanafunzi jinsi ya kukwepa mafataki na vishawishi vyao.

Kwanza wasisimamishwe na kuongea nao, waepuke lifti za bodaboda, bajaj na daladala.

Aidha, wafanyakazi wa taasisi hiyo wanazunguka kutoa elimu kwa wanafunzi wa Mbagala High School, Sekondari ya Mabagala Kuu, Shule za Msingi Mchikichini, Maarifa, Gongo la Mboto JICA na Mwangaza, anasema Mkurugenzi Mtendaji wa WAJIKI, Janeth Mawinza.

Wanashirikiana na wadau wakiwamo polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU, Maofisa wa Maendeleo ya Jamii, na mabalozi wao ambao ni baadhi ya madereva wa bodaboda, bajaj na daladala, anasema Janeth.

Anayeongeza kuwa kurubuniwa kingono wanafunzi na wanawake kumesababisha taasisi hiyo kuanzisha kwa vita na kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', ambayo inaendelea katika shule mbalimbali jijini Dar es Salaam.

"Shida ipo shuleni lakini kwa kiasi fulani tumejitahidi kuwaelimisha wanafunzi ili wajitambue, wawe makini na watu wanaotumia vyombo vya usafiri au fedha kuwarubuni," anasema Janeth.

Mwezeshaji wa WAJIKI, Hans Obote, anasema tangu kuanzishwa 2018, ilifanya kazi Kinondoni, Ilala na sasa Temeke na kwamba inatarajia kufika Ubungo na Kigamboni.




Wanafunzi katika shule za msingi na sekondari wilayani Temeke wakipata elimu kukabiliana na vishawishi vya ngono inayotolewa na WAJIKI. **PICHA: SABATO KASIKA**

### KUJITAMBUA

Mwezeshaji wa mafunzo kwa wanafunzi anasema, wanafanya kampeni ili watambue haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu lakini pia kukwepa vishawishi.

"Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ni wadogo wanashawishika kirahisi, hivyo tunawafundisha kuepuka vishawishi, wasikubali lifti au kupewa fedha na watu wasiowajua," anasema Obote.

"Nasi wadau wa kupinga rushwa hiyo, tumeona kuna haja ya kuzunguka katika shule na kuwaelekeza kujitambua ili wawe makini dhidi ya rushwa ya ngono hatimaye watimize ndoto zao katika elimu," anasema.

Anaongeza kuwa WAJIKI na wadau wapo kwenye kampeni ya shule hadi shule kuelimisha wanafunzi mbinu hizo na madhara ya kuingia kwenye mahusiano wangali wadogo.

"Nasi wadau wa kupinga rushwa hiyo, tumeona kuna haja ya kuzunguka katika shule na kuwaelekeza kutambua viashiria vyote vya rushwa ya ngono ili wawe makini, kwani tunataka watimize ndoto zao," anasema.

### VIKWAZO VIPO

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza, anasema, pamoja na hatua mbalimbali ambazo taasisi yake inachukua ili kumkomboa mtoto wa kike dhidi ya rushwa ya ngono, inakumbana na vikwazo.

Anasema wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hawaoni umuhimu wa kulinda watoto dhidi ya rushwa hiyo hali inayosababisha wasitoe ushirikiano kwa taasisi hiyo.

"Sisi tuna wadau mbalimbali tunaofanya nao kazi na wanaweza kutupa taarifa kuhusu binti anashiriki rushwa ya ngono, tukimpa mzazi taarifa ili tushirikiane kumkamata mtuhumiwa, anakuja juu," anasema.

Kukosekana kwa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya wazazi na walezi katika vita hiyo, ni kikwazo kikubwa kwa taasisi hiyo kufanikisha mapambano ya rushwa ya ngono.

"Ukosefu wa fedha za kutosha, kwani tunawategemea Women Fund Tanzania (WFT) pekee, ni changamoto, lakini tunatamani kupata wadau wengine zaidi ili tuweze kupanua shughuli zetu Dar es Salaam na kwenda mikoa mingine," anasema.

Anaongeza kuwa ingawa wamefanikiwa kupata mabalozi madereva wa bodaboda, bajaj na daladala kusaidiana nao katika mapambano ya rushwa hiyo, wanatamani waongezeke zaidi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata Kibondemaji Mbagala ambako elimu ilitolewa kwa wanafunzi wa Sekondari za Mbagala High School na Mbagala Kuu, Mwajabu Tulian, anaungana na Janeth kuhusu vikwazo vya baadhi ya wazazi na walezi.

"Ni kweli baadhi yao hawaoni umuhimu wa kutoa ushirikiano katika vita hii, wanadhani ni haki watoto wao kuingia kwenye

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Usafiri mabasi ya shule; huduma yenye hofu ya ajali, kuchoka, kukosa usingizi

USAFIRI kwa wanafunzi ni jambo muhimu na lisilokwepeka, ndiyo maana wanaotegemea daladala na usafiri wa umma, safari yao ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani ina matatizo na ni moja ya vyanzo vinavyo wakwamisha kielimu.

Kukosa usafiri wa kuaminika wa shule kwa wanafunzi kunahusishwa na mabinti kupata mimba kisa lifti za bodaboda na huruma za madereva wa magari mengine.

Si hivyo tu, ni chanzo cha watoto kujifunza uhalifu mfano kushiriki ngono na ulawiti, kutumia dawa za kulevya, mirungi, bangi na kupora au udokozi.

Kungoja mabasi muda mrefu na kukatiliwa kupakia kunawakatisha tamaa wakitumbukia pia kwenye mambo yasiyo na tija mfano kujiingiza kwenye kamari, kuwa wateja wa sinema za ngono kwenye vibanda umiza na hata wavulana kuwa na uhusiano wa kingono na wenza walio wazidi umri.

Hayo ni yale yanayowapata watoto wasio na usafiri wa uhakika, lakini jambo ambalo halijazungumzwa ni msururu wa changamoto zinazowakabili wanafunzi wanaosoma shule zenye usafiri na zinazofundishwa kwa Kiingereza.

Wengi wanaziita shule za 'international' lakini jina sahihi ni shule za 'English medium' ambazo licha ya kuwa na usafiri huduma hiyo inaweza kuwatesa wazazi na wanafunzi wake kutokana na mambo mengi, yanayoibuliwa na ufuatiliaji uliofanywa na Nipashe jijini Dar es Salaam.




Usafiri wa kutumia mabasi ya shule wakati mwingine ni kero yanapoharibika na kukwama barabarani. **PICHA MTANDAO**

#### KUHARIBIKA/UBOVU

Shirika la Afya Duniani (WHO) lilishatoa angalizo kuwa duniani kote, ajali za barabarani ni sababu kuu ya vifo vya watoto na vijana wenye umri kati ya miaka 5-29, lakini mabasi ya shule mengi ni mabovu.

Kuna matukio mengi ambayo mabasi ya shule yanakutwa barabarani yameharibika. Msimu wa mvua ndiyo unakuwa hatari zaidi.

Mengine yanatengenezwa kwa siku kadhaa barabarani na machache yaliyoshindikana husogezwa nyumba za jirani kusubiri mafundi yakikaa hata baada ya siku mbili. Kwa ujumla mabasi hayo ni tatizo na pengine hatari kwa watoto.

Kuharibika kunasababisha kuchelewa kufika vituoni, hivyo wazazi, walezi na watoto wao huyasubiri kuanzia saa 11 hadi saa 1:00 asubuhi ndipo uongozi hupiga simu na wazazi kulazimika kukodisha bajaji au pikipiki kuwapeleka wanafunzi shuleni, usalama uko wapi?

> Kukosa magari kunasababisha kazi ngumu kupita kiasi safari ndefu zisizo za lazima watoto kuzunguka sehemu kubwa kwenda shuleni na kurudi nyumbani na kuchoka zaidi.

Lakini ubovu hutokea pia jioni na watoto wakarejea nyumbani saa 2:00 badala ya saa 10.

Kwa hiyo Tanzania inapoelekea kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika wadau watazame usalama wa wanafunzi kuanzia, walimu, walezi, wazazi kampuni za magari na serikali ili kuboresha ustawi wa watoto kwa kufanya usafiri wa shule kuwa salama zaidi.

#### CHANZO CHA HOFU

Kusafiri kwenda shuleni ni sababu ya hofu kwa mzazi, mlezi na mtoto. Shule nyingi inaelekea hazina magari ya kutosha hivyo husababisha safari ndefu sehemu nyingine gari linawachukua watoto saa 11 alfajiri.

Wazazi na walezi hamjiulizi inakuwaje binti yako wa miaka nane unamtoa nyumba saa 11 alfajiri wakati wewe umelala?

Inakuwaje unamkabidhi mtu usiyemfahamu? Asubuhi hiyo dereva wa shule anaweza kuwa anaeendesha gari akiwa peke yake, je, akiweka muziki au video isiyo na maadili mtoto anajifunza nini?

Kukosa magari kunasababisha kazi ngumu kupita kiasi safari ndefu zisizo za lazima watoto kuzunguka sehemu kubwa kwenda shuleni na kurudi nyumbani na kuchoka zaidi.

Uhaba huo husababisha watoto kuamka alfajiri mno hata saa 10 ili kuwahi basi moja la shule, huchoka kwani hurejea nyumbani jioni sana hata saa moja, na kuwanyima muda wa kutosha kukamilisha kazi za shule, kulala na kucheza.

#### KURUNDIKANA

Ufuatiliaji uliofanywa na Nipashe umegundua kuwa ili kuwapeleka watoto wote shuleni kwa wakati kwa ajili ya kuwahi kipindi cha kwanza madereva huchukua wanafunzi wengi wapo wanaosimama, wanaokaa na kukaliana tena wote hawavai mikanda ya usalama, hutembea safari moja ndefu ambayo huwaweka watoto waliopanda mwanzo kukaa zaidi ya saa nne (saa 11 hadi saa 2:30 asubuhi) barabarani. Lakini, pia magari ya shule huendeshwa kwa kasi.

Yote hayo ni kuchoka kwa madereva na wanafunzi pamoja na walimu wanaowasindikiza, inamaanisha pia kwamba wote hawapati usingizi wa kutosha, kutokana na saa wanazopaswa kuamka, kutembea barabarani na kuwahi shuleni kwa wakati.

Mtoto wa Afrika anayesoma English Medium, bado ana kazi ngumu licha ya kwamba ana usafiri.

#### MAMBO YAKUJIULIZA

Shule nyingi hukabiliana na changamoto hizi zinazohatarisha usalama na afya ya wanafunzi wao? Mabasi yenu ni salama au mazima ? Je, shule zina mabasi ya kutosha?

Kwa wazazi na walezi, nyumbani ni mbali sana na shule ambayo mtoto wako anasoma? Unafikiria nini kuhusu kila siku kuamka saa 10 alfajiri?

Yapo madai kuwa madereva wengi ni ndugu na jamaa wa wamiliki wa shule vipi kuhusu madai hayo? Madereva wa shule yako wana taaluma ya udereva? Je, wamefunzwa au ni kupeana kazi kama mwanafamilia? Je, uelewa wao wa masuala ya usalama barabarani ni mzuri kiasi gani? Uendeshaji wao ukoje? Mbona jioni mabasi ya shule yanageuzwa daladala kubeba abiria uongozi wa shule unalifahamu hilo? Kuna usafi wowote hapo? Vipi kuhusu mikanda? Kwanini haitumiki?

#### KWA KAMPUNI

Kampuni za magari zinapaswa kuamka kuangalia namna ya kuandaa mabasi ya wanafunzi badala ya kuacha hali kubaki kama ilivyo. Kampuni zinaweza, kwa mfano, kutoa mikopo nafuu ya magari kwa shule zenye usafiri. Lakini zinaweza kuanzisha utaratibu wa kukodisha magari kwa utaratibu unaonufaisha pande zote.

Hata benki nazo zina mchango wa kushiriki katika kukopesha magari kwa kushirikiana na kampuni za magari na kuweka utaratibu usioumiza wa kulipa magari hayo.

Kwa watunga sera na wasimamizi wake, pamoja na kuagiza magari ya shule kupakwa rangi ya njano na kuandikwa 'school bus' polisi wayakague mara kwa mara na mamlaka nyingine kama LATRA zishirikiane na polisi kuhakikisha usafiri mabasi ya shule hauwi chanzo cha hofu kwa mwanafunzi mzazi, mlezi na jamii.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

INAPOTIMIZA UMRI MIAKA 56

# Jifunze; sura kamili ya BOT, ilikotoka, iliko na inakoelekea

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 1965 na kuanza kazi zake tarehe 14 Juni 1966. Hivyo, ifikapo kila tarehe kama ya leo ni maadhimisho na safari hii inatimu mwaka wa 56 tangu ilipoanza kufanya kazi.

Kuanzishwa BoT, ni hatua uya kimaendeleo kutoka mfumo kama huo wa nchi za Afrika Mashariki. Ni wakati, Tanzania ina imamaka mmoja imeanza kutekiweza mpango wa wake wa kwanza kitaifa wa maendeleo wa miaka mitano tangu kupata uhuru.

Pia ukawa mwaka mmoja wa Muungano na Zanzibar, BOT ikihudumia pande hizo, hali kadhalika taifa likiingia katika mfumo hodhi wa uchumi, kwa kivuli cha sera za Ujamaa.

### MAJUKUMU YA BENKI KUU

Katikia kipindi chote tangu uhuru, BOT imekuwa ikibadilika na sera za uchumi na fedha. Mfumo hodhi wa uchumi uliachwa mwishoni mwea mwaka 1985 na hadi kufikia mwanzoni mwa miaka 1990, kulishuhudiwa mabadiliko makubwa.

Sheria za fedha, benki na mifumo mingine kama ya bima na uuzaji fedha za kigeni, vyote hivyo vikachukua sura mpya chini ya usimamizi wa BOT.

Kulingana na Sera ya Ujamaa, Benki Kuu ilsimamia utoaji ikopo kupanga viwango vya riba na viwango vya kubadilishana fedha za kigeni, hata biashara hiyo.

Pia, nmfumo ukaangukia uchumi unaotegemea nguvu ya soko, serikali ilifanya mageuzi makubwa katika sekta ya fedha hata kushuhdiwa mabadiliko hayo kuanzia miaka ya 1990.

Mapendekezo ya Ripoti ya Tume ya Nyirabu ya mwaka 1991, yakliasema baadhi ya majukumu ya BOT, yalibadilika, hata kubakiwa na: Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei; kuchapisha na kusambaza fedha kwa ajili ya shughuli za kiuchumi, na kusimamia sekta ya fedha.

Aidha, BOT ikawa inafuatilia mwenendo mzima wa uchumi nchiNI na kutoa ushauri kwa serikali, kusimamia mifumo ya malipo ya Taifa, pia kusimamia akiba ya fedha za kigeni iendane na mahitaji ya nchi kwa ujumla.



Majengo ya Benki Kuu ya Tanzania. **PICHA MTANDAO**

Vilevile, inatoa huduma za kibenki kwa serikali na benki na kuwezesha utekelezaji wa sera ya bajeti kwa niaba ya serikali, vyote kwa ujumla wake BOT ikiwajkibikia kuweka mazingira wezeshi kwa shughuli za uzalishaji mali, huduma, biashara na uwekezaji nchini.

### SURA YA MAFANIKIO

BOT katika taarifa yake inasema uchumi umekuwa ukiridhisha sehemu kubwa ndani ya kipindi cha miaka 56 tangu kuanzishwa Benki Kuu, ikitoa mfano miaka 10 iliyopita kabla ya janga la UVIKO-19, ukuaji wa uchumi ulikuwa kwa wastani wa asilimia 6.7.

Hiyo inatajwa kuchukua nafasi, licha ya kuwapo janga la UVIKO-19, ukuaji uchumi ukiwa katika asilimia 4.8 hadi kufikia mwaka 2020, hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizokwepa mdororo wa uchumi.

Hapo BOT inatajwa kuchangia mafanikio ya ukuaji wa uchumi kuputia utekelezaji mzuri wa sera ya fedha, kuhakikisha utulivu wa mwenendo wa bei za bidhaa na huduma.

Pia, inataja utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni, kuwepo ukwasi wa kutosha katika benki nchini kwa ajili ya mikopo ya sekta binafsi, na kutoa ushauri namna bora ya kutekeleza sera za uchumi.

Hivyo, hadi Julai mwaka 2020 Tanzania ilaingia katika daraja, kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati ikiwa na kipato cha mtu mmoja wastani wa dola za Marekani 1,080 kwa mwaka 2019.

Mafanikio pia yanatajwa, kuonekana kasi ya maendeleo ya binadamu (Human Development Index-HDI),ambayo ni katika nyanja kuu tatu; afya; elimu; na viwango vya maisha.

Ripoti ya Shirika la Maendeleo al Umoja wa Mataifa(UNDP) mwaka 2020 ikaonyesha kuongezeka ubora umri wa mtu kuishi kutoka miaka 63.1 mwaka 2015 hadi 65.5 mwaka 2019, pamoja na kuongezeka kwa miaka tarajiwa ya kusoma na pato la kila mtanzania.

> BOT inatamka kudhibiti mfumuko wa bei, licha ya kuwepo kwa changamoto za kiuchumi nchini na duniani katika vipindi tofauti.

### MFUMUKO BEI& MIKOPO

BOT inatamka kudhibiti mfumuko wa bei, licha ya kuwepo kwa changamoto za kiuchumi nchini na duniani katika vipindi tofauti.

Mfano inataja katika miaka 10 iliyopita, mfumuko wa bei uko chini ya asilimia 10, ikibadilika kuoanda na kushuka kwa wastani asilimia 3-5 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Pia, kwa mikopo, BOT inasema imefanikisha kuchangia upatikanaji na ukuaji mikopo kwa sekta binafsi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na hata ukuaji mikopo kwa sekta binafsi kuwa juu, kulingana na malengo yaliyokusudiwa na sera.

### FEDHA KIGENI/THAMANI

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu, akiba ya fedha za kigeni inayosimamiwa na Benki Kuu inatakiwa itosheleze uagizaji bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Hiyo ni kwa makubaliano ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), benki kuu za nchi wanachama zinatakiwa kusimamia kiwango hicho na kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ni miezi sita.

Katika eneo hilo, BOT inaeleza katika miaka 20 iliyopita, hivi sasa akiba iliyopo inatosheleza takribani miezi saba ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi.

Kuhusu mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni BOT inasema uko tulivu, isipokuwa katika vipindi vichache ambapo shilingi inashuka thamani kwa msukumo wa mabadiliko ya uchumi duniani.

Ni hali inayotajwa kuwezesha kuimarisha biashara baina ya Tanzania na nchi za nje, kuvutia uwekezaji na kuimarisha utulivu katika bei za bidhaa na huduma nchini.

### SAFARI SEKTA FEDHA

Sekta ya Fedha inaelezwa imepitia mabadiliko makubwa

INAENDELEA UK.14

# Jifunze; sura kamili ya BOT, ilikotoka, iliko na inakoelekea

INATOKA UK.13

katika miaka 56 ya BOT, ikianzia mwaka 1961 hadi mwanzoni mwa mwaka 1967, ilipofanya kazi na kusimamiwachini ya mfumo wa soko huria, wakati huo sekta hiyo ilikuwa ndogo na sehemu kubwa ikawa ya benki binafsi, kwa maeneo machache mijini.

Baada ya mwaka 1967 hadi mwanzoni mwa mwaka 1991, sekta ya fedha ilijumuisha benki na taasisi za fedha chache chini ya miliki ya serikali, baada ya kutaifishwa mwaka kupitia Azimio la Arusha na kuanza utekelezaji wa sera za Ujamaa na Kujitegemea.

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, sekta ya fedha zilifanyiwa mageuzi makubwa kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1990, ili kuongeza ufanisi na mchango wake katika ukuzaji uchumi, samba na kuendana a mfumo huria kiuchumi.

Ni mageuzi yaliyohusisha maboresho ya sheria za usimamizi wa sekta ya fedha, sera ya soko huria, na kuanzishwa benki na taasisi za fedha binafsi, hata mafanikio makubwa kushuhudiwa mafanikio makubwa, huduma za fedha kuongezeka na kufikia maeneo mengi, tofauti na awali.

Utafiti iliofanyika unaoitwa 'Utafiti Finscope' (2017) unaonyesha huduma jumuishi za kifedha ziliongezeka hadi kufikia asilimia 65 ya watu wazima kutoka asilimia 58 mwaka 2013, ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la huduma za fedha kwa njia ya simu.

Aidha, idadi ya benki ziliongezeka kwa kiasi kikubwa kufikia 46, kutoka takriban benki sita za mwaka 1991 na sekta ya benki ikiwa imara zaidi, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha na kuhimili misukosuko ya ndani na nje.

Pia, inataja masoko ya fedha yameanzishwa, ikiwemo ya dhamana za serikali, soko la fedha za kigeni, na soko la hisa na mitaji. Masoko hayo yameenda sambamba na kuanzishwa vyombo vya usimamizi, ikiwemo Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

Yote yanatajwa kuiwezesha serikali sekta binafsi kuweza kukopa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, wakilenga wawekezaji, masoko haya yametoa fursa za kupata mitaji na kukuza kipato.

Vilevile, masoko yameanzishwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji sera ya fedha na kuwezesha benki kupata ukwasi wa kutoa mikopo na shughuli za maendeleo.

Hadi sasa BOT imeanzisha matawi katika kanda mbalimbali nchini, ili kusogeza huduma zakwe, mbaloi na makoa makuu yaliyokuwa jijini Dar es kabla ya kuhamishiwa jijini Dodoma mwaka 2020, mtandao uko katika maeneo yafuatayo na mwaka wa uanzishajki kwenye mabano: Arusha (1977), Mwanza (1980), Mbeya (1988), Dodoma (2015) na Mtwara (2016).

Tawi la Zanzibar lilianza kama kituo cha usambazaji sarafu mwaka 1967 kabla ya kuwa tawi kamili mwaka 1988.

BOT inashiriki kwenye Kamati ya Masuala ya Fedha ya magavana wa benki kuu za nchi wanachama wa EAC, zikitekelezwa kwa Itifaki za pamoja:Umoja wa Faorodha, Soko la Pamoja, na Umoja wa Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Vivyo hivyo BOT ni Mjumbe wa Kamati ya Magavana wa Benki Kuu (CCBG) katika Jumuiya ya Nchi Wanachama wa SADC kamayo inayoweka mikakati ya kuendeleza sekta ya fedha na kukuza uchumi kwa nchi wanachama.

### CHANGAMOTO ZAKE

Benki Kuu inataja changamoto zake katika utekelezaji majukumu yake tangu kuanzishwa kwake mwaka 1966, ni katika mwenendo wa uchumi wa dunia, mabadiliko ya tabianchi na majanga mbalimbali.

"Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kupanda mara kwa mara kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, ukame kwa baadhi ya miaka, mdororo wa uchumi duniani mwaka 2009.

"Mdororo wa uchumi barani Ulaya mwaka 2012, na janga la UVIKO-19. Vilevile, kumekuwepo na changamoto ya viwango vya riba kubaki juu na viwango vya juu vya mikopo chechefu, japokuwa vimekuwa vikishuka," inatamka taarifa yake.

BOT inasema kwa kushirikiana na serikali na wadau wa maendeleo, inachukua hatua za kupunguza madhara katika uchumi na utekelezaji wa majukumu yake, ikitoa mfano wa mkasa wa janga la UVIKO-19 nahatua za kisera dhidi yake.

### INAKOELEKEA

BOT inatamka kupanga kuendelea kuchukua hatua za kudumisha ufanisi na kuongeza ubunifu katika utekelezaji wa majukumu yake, akifafanuia katika taarifa yake:

"Juhudi hizi zinahusisha matumizi ya teknolojia, kujenga uwezo wa wafanyakazi ili kuongeza tija, kufanya tafiti na kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi."

Hadi sasa inataja kunuia katika kuwepo ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, na kuhakikisha kuwa viwango vya riba vya mikopo vinaendelea kupungua na kupunguza mikopo chechefu.

## WANENAVYO MALENGA

### KURA NI SAWA NA HEWA

Ndio thamani ya kura, inayowafanya kula,
Yafanana barabara, toka Kyerwa hadi Kyela,
Hakuna iliyo bora, au ya kufunga tela,
Kura ni sawa na hewa, mtu moja kura moja.

Kura haina ubora, sawa sawa na chakula,
Kula tumbo litafura, baadaye choo jela,
Yule ulimpa kura, kesho akuona fala,
Kura ni sawa na hewa, mtu moja kura moja.

Sirini hata hadhara, mpini ule wa kula,
Akishika yeye bora, wengine wote hewala,
Hapo kutambia kura, hakuna nenda kulala,
Kura ni sawa na hewa, mto moja kura moja.

Haina elimu kura, picha kamili trela,
Peleka kule busara, kura kichwa inakula,
Ina raha na madhara, dhahabu rungu la dola,
Kura ni sawa na hewa, kura moja mtu moja.

Idadi ya watu bora, waamke si kulala,
Inuka umwage sera, jioni kafanye sala,
Ridhisha wakupe kura, kwa furaha utalala,
Kura ni sawa na hewa, kura moja mtu moja.

Elimu haina dhara, shangingi na daladala,
Digrii za kukera, huwezi pata chakula,
Wewe chakurachakura, kura pata utakula,
Kura ni sawa na hewa, kura moja mtu moja.

Ujue kujenga sera, au rasta msela,
Mapinduzi hizo kura, mwingine ambwelambwela,
Utaziona ishara, mbio aenda kulala,
Kura ni sawa na hewa, kura moja mtu moja.

Wanaoleta madhara, na kura kuwa jalala,
Wajidaio imara, milele wao ni kula,
Wanafanya ya kukera, hata kuleta msala,
Kura ni sawa na hewa, kura moja mtu moja.

Vizuri zapigwa kura, wenye suti na madela,
Kura haijali sura, nani kingi anakula,
Wanaoleta hasira, kura kufanywa tambala,
Kura ni sawa na hewa, kura moja mtu moja.

Hebu iacheni kura, watu wapate chakula,
Wakitumika ni bora, haki ni kama besela,
Kuzichanachana kura, kero huleta kuzila,
Kura ni sawa na hewa, kura moja mtu moja.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### INAHITAJIKA NGUVU

Inahitajika nguvu, kutoa kilicho ndani,
Kama ukiwa mvivu, kitabaki kule ndani,
Lazima uone wivu, wewe ushindwe kwa nini,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Bila kupasua yai, kikuku chafia ndani,
Kwa nje ni zuri yai, japo lakosa thamani,
Kifaranga kwenye yai, hicho ndicho cha thamani,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Mungu kakupa uwezo, wa mambo mengi kubuni,
Ukiufanya mchezo, yatabaki mawazoni,
Litendee kazi wazo, ujiongeze thamani,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Ninajua biashara, huo wako ujivuni,
Na kwamba kwako hasara, inabaki kitabuni,
Lakini kuuza sura, kwa nje waona soni,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Jipapatue kidogo, uingie darasani,
Usome japo kidogo, ndipo uende kazini,
Ukikumbana na gogo, jua kupitia chini,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Kama mtu kasimama, jua kakwepa mipini,
Kunakuwa na kukwama, kuteleza hadi chini,
Lakini anachagama, lengo liwe mkononi,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Unaweza ukakwama, usiishie njiani,
Mashua kwenda mrama, ni mambo ya baharini,
Jitahidi fanya hima, ufikie kileleni,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Mama kuzaa mtoto, anakuwa hatarini,
Akifanya ya kitoto, twamzika kaburini,
Ila ajitia joto, toto laja duniani,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Jikakamue mwenzangu, shika jembe la mpini,
Kama jembe ni kiwingu, biashara iwe dini,
Chapa kazi ndugu yangu, mali mwako mkononi,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

Mimi najitia nguvu, nisiishie njiani,
Ikibidi kwa mabavu, lengo liwe mkononi,
Nicheke vunja na mbavu, nasepa barabarani,
Kifaranga kutokeza, inahitajika nguvu.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





## Watanzania watakiwa kutumia mitandao kusaidia jamii

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibango, amewaomba Watanzania kuitumia mitandao ya mawasiliano kwa malengo ya kujiletea maendeleo na kusaidia jamii.

Alitoa rai hiyo wakati akipokea na kukabidhi misaada ya nguo iliyotolewa na kikundi cha wanawake Itambue Thamani Yako (ITY) kwa ajili ya wanawake wajauzito na watoto walioko Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Chibango aliitaka jamii kuhakikisha wanabadilika katika matumizi ya mitandao ili iweze kuwaletea maendeleo ya kiuchumi.

Chibango alisema kuwa kikundi hicho cha wanawake cha Itambue Thamani Yako, kimefanikiwa baada ya kuungana na kuamua kuunda kikundi ambacho hivi sasa kimekuwa kikitoa misaada mbalimbali kwa jamii.

"Wanawake hao kweli hawana budi kuigwa mfano ambao tunaoshuhudia hapa leo maana wameungana kupitia mitandao ya simu na kuamua kuunda kikundi ambacho kinachosaidia jamii ikiwamo kwenye hospitali.

"Hivyo niwaombe Watanzania hususani vijana wa kike na kiume, simu zao zitumike kwa malengo ya kimaendeleo na kiuchumi, badala ya kuangalia picha ambazo hazina tija kwa upande wao na hata kwa jamii,"alisema.

Katibu wa kikundi hicho, Jackline Nanyaro, akizungumza wakati akikabidhi misaada hiyo, alisema kuwa wameweza kufanikisha baada ya kuungana kwa pamoja kwa njia ya mitandao.

Nanyaro alisema walitumia mawasiliano yao kama sehemu ya kuweza kukutana kwa pamoja na wakaamua kuunda kikundi ambacho kitafanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo cha kutoa misaada kwenye maeneo mbalimbali.

"Mpaka sasa kikundi chetu tumeweza kuwafikia jamii mbalimbali ikiwamo ya wafungwa magerezani, wagonjwa hospitalini na kwenye vituo vya watoto yatima kwa kuwapelekea misaada kama tulivyo fanya hapa,"alisema.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Watoto wa Hospitali ya Rufani Dodoma, Dk. Enid Chiwanga, alisema kwa mara ya kwanza wanapokea msaada kutoka kwenye kikundi kilichoungana kupitia mitandao.

"Hivyo ni wakati sasa jamii ya Watanzania kuachana na tabia ya kuitumia mitandao kama sehemu ya kuangalia na kusoma vitu visivyofaa, badala yake watumie kwa manufaa kama ilivyo kwa kikundi hiki ambacho leo hii wameungana na kuweza kutoa misaada mbalimbali," alisema Dk. Chiwanga.

# Serikali yashauriwa kuvitumia vyuo vya kilimo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuvitumia vyuo vya elimu ya kilimo nchini kuwajengea maarifa vijana ili wajiajiri na kuondokana na dhana ya kusubiri kuajiriwa na serikali.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini Dodoma na Mhitimu wa Chuo cha Kilimo Uyole mkoni Mbeya, Christopher Dioniz, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya elimu ya mafunzo ya ufundi na ufundi stadi.

Dionizi alisema ipo haja kwa serikali kuwekeza nguvu katika vyuo vya kilimo ili vitumike kuwajengea uwezo vijana wa kujiajiri katika sekta hiyo na kutumia fursa zilizoko nchini.

Alisema kupitia vyuo hivyo vijana wengi watapata fursa ya kujiajiri kupitia kilimo na kuzalisha malighafi kwa ajili ya kulisha viwanda vya ndani na nje ya nchi.

"Kilimo ndiyo sekta inayoongoza kwa kuchangia pato la taifa, lakini inatumika kwa ajili ya kuleta uhakika wa chakula nchini, hivyo ikitumika ipasavyo itasaidia kutoa ajira kwa vijana.

"Mimi nilihitimu katika Chuo cha Uyole na mafunzo niliyoyapata pale yameniwezesha kujiari mwenyewe na kuajiri wengine kupitia shughuli za kilimo na ufugaji, lakini pia nimenufaika mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri kupitia kazi zangu za kilimo na ufugaji,"alisisitiza Dioniz.

Alisema anaipongeza serikali kwa kuongeza bajeti ya kilimo katika mwaka huu wa fedha ambayo itakwenda kujibu maswali mengi yaliyokuwa yakiwasumbua wakulima.

"Vijana wanapaswa kuitumia fursa hii kujiajiri kwa kilimo cha mboga na matunda ambacho pia bajeti ya mwaka huu wa fedha imetengewa kiasi kikubwa cha fedha,"alisema Dioniz.

Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, hivi karibuni alisema serikali imeweka mkakati kwamba hadi ifikapo mwaka 2030 iwe imesafirisha nje mboga na matunda yenye thamani ya Sh. bilioni mbili.

Alisema ili kufikia ajenga ya mwaka 2030 kunatakiwa kuwapo kwa utaishi mkubwa wa kisiasa katika kuendeleza sekta ya kilimo nchini.




Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Watoto Hospitali ya Rufani ya Dodoma, Dk. Enid Chiwango (kulia), akipokea msaada wa mashuka yaliyotolewa kwa ajili ya wodi ya wajawazito na watoto kutoka kwa Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, yaliyotolewa na Kikundi cha Wanawake cha Itambue Thamani Yako juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wanaotumikisha watoto, kuwanyima haki kusakwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye ulemavu, Patrobas Katambi, amesema serikali itaendelea kuwasaka watu ambao wamekuwa wakiwatumikisha watoto na kuwanyima haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu.

Alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika maadhimisho ya Siku ya Kupinga Utumikishwaji wa Watoto Duniani.

Katambi alisema serikali inafuatilia kwa karibu watu ambao wamekuwa wakijihusisha na masuala ya ajira kwa watoto ili kuwachukulia hatua za kisheria.

Alisema ajira kwa watoto imekuwa na madhara makubwa kwa taifa, hivyo serikali itaendelea kuongeza umakini katika kuwafuatilia na kuwachukulia hatua kali wote watakaobainika kutumikisha watoto.

Aidha, alisema moja katika eneo ambalo wanalifutilia kwa karibu ni wafanyakazi wa ndani ambao wamekuwa wakipitia manyanyaso makubwa kutoka kwa waajiri wao kwa kufanyia ukatili wa kijinsia.

"Wasichana wa kazi wanapata shida sana wamekuwa wakinyanyaswa sana na mabosi wao wanapigwa, wanabakwa na wengine kupatiwa ujauzito na ndugu wa karibu katika nyumba ambayo wanafanya kazi," alisema Katambi.

Kadhalika, alisema vitendo vya utumikishwaji wa watoto vimekuwa na madhara makubwa sana kwa taifa ikiwamo kuongezeka kwa umaskini.

Katambi alisema madhara mengine ni kuwa na taifa la watu wengi wasiojua kusoma na kuandika kutoka na watoto wengi kufanya kazi badala ya kwenda shule. Alisema: "Pia kuenea kwa magonjwa mbalimbali ikiwamo Ukimwi hasa kwa mabinti wanaofanya kazi za ndani kurubuniwa na wengine kupata ujauzito na kupoteza ndoto zao".

Vilevile, alisema watoto wengi wanaofanya kazi wamekuwa wakipata ulemavu kutokana na mazingira wanayofanyia kazi kuwa siyo rafiki kwao.

Mwenyekiti wa mtandao wa mashirika ya kupinga ajira kwa watoto, Scholastica Pembe, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuwaleta pamoja wadau wote wa kupinga vitendo vya utumikishaji watoto.

Alisema mtandao huo hivi sasa una wanachama zaidi ya 40 Tanzania Bara na Zanzibar, wakiwa na lengo la kushikamana pamoja ili kukomesha vitendo vya utumikishaji wa watoto nchini.



# Wakulima walalamika kupaa bei pembejeo za kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa viazi mviringo katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wamesema mabadiliko ya tabianchi na kupaa kwa bei ya pembejeo za kilimo hususani mbolea, vimesababisha kushuka kwa mavuno yao.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo maalumu ya athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye kilimo yaliyoandaliwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali lenye asili ya nchi ya Uholanzi lijulikanalo kwa jina la SNV kupitia mradi wake wa CRAFT na kushirikisha wadau mbalimbali wa kilimo.

Walioshiriki kwenye mafunzo hayo ni wakulima, maofisa kilimo, kampuni zinazouza pembejeo za kilimo, wanunuzi wa viazi pamoja na watafiti wa kilimo kutoka katika taasisi mbalimbali za serikali na zisizokuwa za serikali.

Mmoja wa wakulima hao, Faustine Kilumila, alisema miaka yote walikuwa wanapanda viazi mwezi Machi na vilikuwa vinakomaa kutokana na uwapo wa mvua, lakini kwa mwaka huu hali ni tofauti kutokana na mvua kuisha mapema.

Alisema hata msimu wa baridi kali ambayo ilikuwa inaathiri viazi ilikuwa inaanza Julai, lakini mwaka huu hali ni tofauti kutokana na kuanza mapema na hivyo kuathiri zao hilo na kuhatarisha uchumi wao.

"Mwaka huu viazi ambavyo tulipanda mwezi Machi vinahitaji kuanza kumwagiliwa wakati miaka iliyopita vilikuwa vinakomaa vizuri, lakini barafu zimewahi mno maana ilikuwa inaanza Julai ila mwaka huu imeanza Juni, na bahati mbaya ni kwamba barafu haina dawa," alisema Kilumila.

Naye Stella Mwamakula alisema mwaka huu bei ya mbolea iko juu kuliko miaka yote na wakulima wengi kushindwa kumudu kununua hali iliyowafanya waendelee kulima kilimo cha asili ambacho tija yake ni ndogo.

Alisema miaka ya nyuma mbolea ya kupandia walikuwa wananunua mpaka Sh. 40,000 kwa mfuko wa kilogramu 50, lakini mwaka huu, wamenunua kwa zaidi ya Sh. 120,000.

Meneja wa Huduma za Hali ya Hewa ya Kilimo kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Isaack Yona, alisema mabadiliko ya tabianchi yanayoonekana sasa hivi yataendelea kuleta athari kwa miaka mingine 20 ijayo.

Alisema kwa kawaida uzalishaji wa viazi hutegemea hali ya ubaridi na mvua za wastani, lakini kwa sasa imekuwa tofauti kutokana na kuongezeka kwa joto na kupungua kwa mvua.

"Kwa sasa mvua imepungua kwa kiasi kikubwa na joto limeongezeka sana kiasi kwamba linaathiri uzalishaji wa mazao hasa viazi, madhara ya mabadiliko haya yataendelea kwa miaka kadhaa ijayo," alisema.

Meneja wa Mradi wa CRAFT Tanzania, Menno Keizer, alisema waliamua kufanya mkutano na wakulima pamoja na wadau ili kuelimishana namna bora ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye uzalishaji wa viazi.

Alisema kwa sasa wanawafundisha wakulima kulima kilimo mbadala ikiwamo cha umwagiliaji ili uzalishaji uendelee kuwa wa kiwango cha juu kinachoendana na mahitaji ya soko.

Akifungua mkutano huo, Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, alisema serikali inaendelea na mikakati ya kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa tija na kupata masoko ya uhakika.

Alisema moja kati ya mikakati ya serikali ni kuhakikisha pembejeo za kilimo zinapatikana ikiwamo mbolea na kwa mwaka huu bei ya baadhi ya pembejeo hizo imeathiriwa na vita vya Ukraine na Urusi pamoja na mlipuko wa Virusi vya Corona.



Mchuuzi wa samaki mjini Bunda mkoani Mara, akianika dagaa kwenye vipande vya mifuko ya viroba, mwishoni mwa wiki. Baadhi ya wachuuzi wamekuwa wakitumia njia hiyo ili kuepuka dagaa kuwa na mchanga. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Wanahabari wakumbushwa kufuata sheria, taratibu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAANDISHI wa habari nchini wametakiwa kuandika habari kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa ili kuepuka kuingia kwenye migogoro isiyokuwa na ulazima.

Mwanasheria wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Paul Malimbo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo ya pamoja ya mambo ya sheria kati ya waandishi wa habari na maofisa habari wa mikoa na Halmashauri za mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema waandishi wa habari ni daraja kati ya jamii na serikali na lazima wafanye kazi kwa weledi ikiwa ni pamoja na kuzingatia mipaka ya kazi yao ili kuepuka kusababisha matatizo ikiwamo machafuko kwenye jamii.

"Wanahabari mna wajibu wa kutekeleza majukumu kwa kushirikiana na maofisa habari ili kuhakikisha habari zenu hazileti mashaka kwa wasikilizaji, wasomaji na watazamaji, hivyo hakikisheni mnafanya kazi bila kuondoka kwenye misingi," alisema Malimbo.

Alisema Watanzania hawana nchi nyingine ya kwenda endapo machafuko yatatokea ni lazima misingi ya sheria ifuatwe kuepusha matatizo.

Akiwasilisha mada ya mabadiliko ya sheria, wakili wa kujitegemea, Jebra Kambole, alisema waandishi wanatakiwa kufahamu mabadiliko ya sheria mpya ya Huduma ya Vyombo vya Habari ili kuepukana na madhila ambayo yanaweza kuwapata.

Alisema serikali imetoa nafasi kwa wanahabari kutoa maoni juu ya mabadiliko ya sheria hiyo na kuwataka kuitafuta na kuisoma ili wachangie kitu ambacho wanakijua vizuri.

Aliwataka wanahabari na wadau mbalimbali wa habari kushiriki katika kupigania haki za upatikanaji wa habari na kuhakikisha wanashiriki kwenye mabadiliko yoyote ya sheria.

# Kampuni zapewa siku 21 kuwasilisha taarifa BRELA

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni nchini (BRELA), imewataka wamiliki wa kampuni, kuwasilisha taarifa zao za umiliki, ndani ya siku 21, zifanyiwe kazi ya utambuzi na msajili kwa mujibu wa sheria ili wafanye kazi zao kwa uhuru kabla ya kuchukuliwa hatua.

Maelekezo hayo yalitolewa juzi na Kaimu Mkuu wa sehemu ya kampuni kutoka BRELA, Leticia Zavu, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wamiliki wa kampuni, wanasheria na washauri wa biashara mkoani hapo namna ya kutambua umuhimu wa kusajili shughuli zao.

Zavu, aliwaeleza washiriki hao umuhimu wa dhana ya wamiliki manufaa katika kuhuwisha taarifa za kampuni ili kupata zote za waliokwisha kujisajili BRELA na kujua wanufaika halisi wa hisa zinaonekana kwenye daftari la msajili wa kampuni kutambua mnufaika halisi wa hisa hizo.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili, Kanda ya Mbeya, Alfredy Chapa, alisema serikali imeboresha sheria ya kampuni ili kudhibiti baadhi ya mambo ikiwamo utakatishaji wa fedha na vitendo vingine vya rushwa.

"BRELA kwa kushirikiana na wataalamu Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, iliunda kanuni ya kudhibiti mianya ya rushwa, vitendo vya ugaidi utakatishaji wa fedha kwa kampuni zote zilizosajiliwa," alisema Chapa.

Ofisa Biashara Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, aliiomba BRELA kuweka taarifa zake kwa lugha ya Kiswahili ili iwe rahisi kwa wamiliki wa kampuni kujaza taarifa zote zinazohitajika wakati wa usajili.

Alisema kwa kufanya hivyo kutaongeza mwamko wa wamiliki kutoka maeneo mbalimbali nchini kujitokeza kujaza taarifa zao kwa sababu lugha itakayotumika ni ya Kiswahili.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo akiwamo Kassim Mpika, alisema mafunzo hayo yamekuwa na tija kwao kwa kuwa wametambua utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa ili kumiliki hisa kupitia kampuni zao.

Naye Wakili wa kujitegemea mkoani Mbeya, Salome Mwakalonge, alisema umuhimu wa kujaza taarifa za umiliki wa kampuni kupitia BRELA una lengo la kudhibiti mianya ya rushwa na kuongeza pato kwa serikali ili fedha zinazopatikana zitumike kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Hata hivyo, katika kusogeza huduma za usajili wa kampuni, biashara na leseni, BRELA, imekasimu madaraka kwa maofisa biashara wa mikoa kusimamia zoezi hilo.





Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Mjini Wingwi wakivuka daraja kuelekea shule, kabla ya daraja hilo walishindwa kwenda shule. **PICHA: SELEMANI SULEIMAN**

# Ujenzi wa daraja wapunguza utoro wanafunzi

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa daraja la muda linalounganisha vijiji vya Chupwe, Sebudawa na Mjini Wingwi, kumepunguza utoro wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Mjini Wingi, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kijijini hapo, mwalimu wa dhamana wa shule hiyo, Juma Khamis Kombo, alisema kabla ya kujengwa kwa daraja hilo, utoro wa wanafunzi ulikithiri kutokana na kukosekana kwa kivuko cha uhakika kinachounganisha maeneo hayo.

Alisema baada ya kukamilika kwa daraja hilo lililojengwa kupitia miradi ya jamii uliolibuliwa na wananchi wa shehia hiyo, mahudhurio ya wanafunzi wanaohudhuria shuleni yameimarika.

"Awali wanafunzi walikuwa wanashindwa kufika shule kikawaida kutokana na kushindwa kuvuka kutoka katika makazi yao na kwenda shule hasa katika msimu wa mvua," alieleza mwalimu huyo.

Awali, alisema wananchi walipanga magogo ili kuvuka kutoka eneo moja kwenda jingine kwa ajili ya shughuli za kijamii wakiwamo wanafunzi ambao wengi wao walikuwa wakianguka na madaftari yao kuingia maji.

Alisema shule hiyo iliyoko katika Wilaya ya Micheweni Pemba, yenye wanafunzi 1,272, watoro 118 walirejeshwa shule kupitia mradi wa urejeshaji wa wanafunzi shule unaoendeshwa na Wizara ya Elimu Zanzibar, kabla ya wastani wa 500 walikuwa hawahudhurii shule kikawaida.

"Wanafunzi waliorejeshwa tulionao sasa ni wavulana 670 na wasichana 15 ambao walikuwa wakijihusisha na shughuli mbalimbali zikiwamo za uvuvi na kilimo cha mwani, lakini sasa wapo shule na baadhi yao tumewafanyia mitihani, wanaendelea vyema," alisema.

Baadhi ya wananchi, waliipongeza serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kwa kuwajengea daraja hilo lenye urefu wa zaidi ya mita 60 linalopita juu ya bwawa la maji bahari linalotenganisha vijiji hivyo.

"Kabla ya ujenzi wa daraja hili watoto wetu waliokuwa wakipita hapa kwenda shule huloa na wengine huanguka na kuumia, lakini sasa tunashukuru wanapita kwa amani wakati wa kwenda na kurudi shule," alisema Fatma Hassan Ali, mkazi wa kijiji hicho.

Aidha, aliiomba serikali kuwajengea daraja la kudumu kutokana na lililoko lilijengwa kwa miti kuchakaa na kuwarudisha katika dhiki ya awali.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Miradi ya Jamii (CMC) katika shehia hiyo, alisema awali kabla ya ujenzi wa daraja hilo kulikuwa na kikwazo kikubwa kwa wananchi hasa wanawake na watoto kuzifikia huduma zikiwamo za afya au elimu.

Alisema kuwa hali hiyo iliwalazimu kupita katika eneo lingine ambalo ni masafa marefu kufika kwenye huduma hizo hali iliyobadilika mwaka mmoja na miezi minne baada ya TASAF kugharamia ujenzi huo na kuwataka wananchi kulitunza daraja hilo ili kutumika kwa muda mrefu.

"Hivi sasa tunataka tuanze harambee kwa ajili ya ujenzi wa daraja la kudumu ili kusaidia kwa kizazi cha sasa na kinachokuja kwa sababu eneo hili limezungukwa na bahari hivyo tunahitaji kivuko cha kisasa chenye ubora wa kudumu," alisema.

Kwa upande wake, Kaimu Sheha wa shehia ya Mjini Wingwi, Hussein Makame Hamad, alisema kufunguliwa kwa daraja hilo kumerudisha furaha ya wananchi wa shehia hiyo na kusisitiza haja ya kujengwa kwa daraja la kudumu.

Aidha, Sheha Hamad, aliwataka watu wenye uwezo na viongozi wa jimbo hilo kusaidia ujenzi wa kudumu wa daraja hilo na ujenzi wa barabara ili kuimarisha maendeleo ya kijiji hicho.

Wastani wa Sh. milioni 7.3 zimetumika katika ujenzi wa daraja hilo na uimarishaji wa mazingira ya eneo hilo na zaidi ya miti ya mikoko 3,000 imependwa na wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini.

# 'Wazazi fuatilieni mienendo ya watoto wenu'

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI wametakiwa kuangalia mienendo ya watoto wao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo, ili kuwakinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Hayo yalisemwa na baadhi ya wazazi wa watoto wa Shule ya Sekondari Glorious mjini hapo, wakati walipokuwa wakipatiwa elimu ya udhalilishaji na maofisa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Asia Ali, alisema baadhi ya wazazi huwakaripia watoto jambo ambalo linawafanya kushindwa kusema changamoto zinazowakabili wanapopatwa na matatizo.

Alisema ni vyema kwa wazazi kushirikiana kwa pamoja na kurejesha malezi ya zamani katika kuwalea watoto kwa kuwa nao karibu na kuwaelewesha kuliko kuwakaripia.

Aliwashauri wazazi wenzao kupunguza muhali na kwenda kutoa ushahidi mahakamani pindi masuala hayo ya udhalilishaji yanapotokea.

Pia, aliomba serikali kupitia marekebisho ya sheria kwa kuwekwa adhabu sawa kwa wanaofanya vitendo hivyo kwa mwanamume na mwanamke na kuwekwa adhabu ya kifungo cha maisha au kuuawa.

Naye mwanaharakati wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, Sharifa Abeid Salum, aliwaomba wazazi hasa wanawake kuwachunguza watoto wao na kubaini nyendo zao na kuzijua changamoto zao.

# SMZ yatoa bil. 3.6/- kupunguza makali bei ya mafuta

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imesema bei za mafuta katika soko la dunia zimeendelea kuongezeka, lakini Serikali ya Zanzibar, inaendelea kupunguza makali ya bei hizo kwa kufidia jumla ya Sh. bilioni 3.6 kwa Mei katika bidhaa zote za mafuta.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano, Mbarak Hassan Haji, kutoka mamlaka hiyo aliyasema hayo wakati akitangaza bei za mafuta kwa vyombo vya habari ofisini kwake Maisara zilizoanza kutumika Juni 9, mwaka huu.

Mbarouk alisema, serikali inaendelea kufidia bei ya mafuta kwa wananchi wake ili kupata huduma hiyo kwa urahisi.

Alisema mafuta ya petroli kwa Aprili na Mei yalikuwa yakiuzwa kwa Sh. 2,642 na mwezi huu kabla ya fidia mafuta hayo ilitakiwa yauzwe kwa Sh. 2,924 na baada ya serikai kufidia yanauzwa kwa Sh. 2,800 na serikali imefidia Sh. 124 kwa kila lita moja ya mafuta hayo.

Mbarouk alisema kwa upande wa dizeli bei ya mafuta kwa Aprili na Mei yakiuzwa kwa Sh. 2,644 na kabla ya fidia yalikuwa yauzwe Sh. 3,582 na baada ya serikali kufidia sasa yanauzwa kwa Sh. 2,820 huku serikali ikifidia Sh. 762 kwa kila lita.

Kwa upande wa mafuta ya taa, alisema bei ya Aprili na Mei ilikuwa ni Sh. 2,173 huku kabla ya fidia kwa mwezi huu ilitakiwa iuzwe kwa Sh. 2,782 kwa lita na baada ya fidia itauzwa kwa bei hiyo hiyo.

Alisema matumizi ya jumla wanayotegemea kwa mwezi huu ni karibu lita milioni 18 na wastani ni lita milioni 15, lita milioni 10 kutumika kwa mafuta ya petroli, lita milioni saba diseli na mafuta ya taa.

Akizungumzia sababu za kupanda kwa bei hizo, alisema ni pamoja na kubadilika kwa wastani wa bei za uuzaji wa bidhaa hizo katika Soko la Dunia pamoja na soko la ndani kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Hata hivyo, alisema ZURA inapanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta duniani kwa mwezi uliopita, ili kupata kianzio cha kufanyika mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi huu.

"Tumekuwa tukisisitiza suala la risiti kwa muda mrefu na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), wameanza kulifuatilia hilo katika masuala ya kodi, lakini risiti inabaki kuwa ni kielelezo iwapo mwananchi atapata changamoto yoyote katika kituo cha mafuta," alisisitiza.

Mbarouk aliwahamasisha wananchi kutumia nishati mbadala ikiwamo gesi kwa kupikia badala ya kuni na mkaa ambayo ni adui wa mazingira.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**WILSON SAILES KIMAMLA,** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne na Kidato cha Sita, Kidato cha Nne index **No S.0177/0034** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya Secondary St Mary's Juniour Seminary Mwaka 2013. Kidato cha Sita Index **No S.4405/0573** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya Sekondary St Amedeus Sekondary School Mwaka 2016. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chchote cha Polisi.

**Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/227235/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**RUFAA NAMBA 121 YA 2021**
**(Rufaa hii inatokea baraza la kata kanga katika kesi namba BK/14/2021)**
**AUGUST P. MPOLO........................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**HUSSEIN S.MBUGI..................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe **4/07/2022** mbele ya Mwenyekiti M.Khasim wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautohudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe **13/06/2022**

M. KHASIM
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 85/2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ERNEST YUSTO MGONHO OF NKUHUNGU AREA WITHIN DODOMA REGION**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MKOMENI ERNEST MGONHO**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **28th Day of June, 2022.**

**Dated at Dodoma this 3rd day of June, 2022**

..................................................
**PETITIONER**

**Presented for filling this 13th day of June, 2022**

..................................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VICKY LAWRENCE MSHANGA** anatangaza kupotea kwa kadi za gari zenye usajili namba **T878 AGB na T406 DCF.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/232992/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MASHAKA PETER MWAMAGE ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya GARI yenye namba za usajili **T 832 ASR.** Chassis namba: **SE28TN303802** Injini namba: **R2730332** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/69986/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR

**LESIKAR KILAMIAN SINGOOI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Tractor yenye namba za usajili **T 330 BHG – MASSER FERGUSON.** Chassis namba **MF203480P32825.** Engine namba **2038MF33688F.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/232219/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HUSSEN ROBERT** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.103 CUQ.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. **CONTROL No. 9910833067093.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI NA 09/2022**
**DERICK VICENT.............1. MDAI**
**MATHAYO A. JALLY................2. MDAI**
**DHIDI YA**
**PATHEC LIMITED.....................MDAIWA**
**KWA: PATHEC LIMITED**

**POPOTE MULIPO**

Mnafahamishwa kwamba wadai wamefungua shauri la madai tajwa hapo juu katika Mahakama hii na limeshasikilizwa na sasa lipo katika hatua ya uamuzi.

Hivyo shauri hilo limepangwa hukumu mnamo tarehe 15/06/2022 saa 02:30 asubuhi na mnatakiwa kuwepo, kusikiliza uamuzi dhidi yenu katika madai haya kama sheria inavyoelekeza.

**ZINGATIA KWAMBA,** Kutofika kwenu tarehe hiyo Mahakama itaendelea na hatua hii na kutoa uamuzi bila uwepo wenu.

**IMETOLEWA,** na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 05 Mwaka 2022.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**No.75 of 2022**
**In the matter of the Estate of the late ERNEST RAPHAEL MTILI of Iyumbu within Dodoma City Council.**
**AND**
**In the matter of an application for letters of administration by STELLA JONATHAN SABUNI.**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 10 Day of 06, 2022

**Dated at Dodoma this 06 day of 07,2022**

RESIDENT MAGISTRATE

PRINCIPAL / SENIOR / RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT COURT

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SYLVESTER ERNEST** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA DIPLOMA KILICHOTOLEWA NA ILEMI POLYTECHNIC COLLEGE MWAKA 2015 CHENYE NAMBA IPC/GA/D/2012/04/021.

YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU

**POLISI TAARIFA NJ/A.17/14/VOL/M/31**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**
**Kituo cha MAKOLE, Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 56/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU PRISCA ELSAFI wa IHUMWA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ALHADHIRI FADHIL**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imtolewa leo tarehe 10/06/2022.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**NAZALENA LAMECK NGENZI**

Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha chuo chenye REG NO:REG NO.MNMA/SS/4418/11 Kilicho tolewa na Chuo kikuu cha mwalimu nyerere mwaka 2013 Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi au

**piga simu 0746495921/0765363017**

**DSM/PHQ/RB/228649/2022**

---

**FORM 84**

**NOTICE TO CREDITORS**
**(Rule 111)**

**NOTICE** is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above , named **Mr. WILBERFOCE AMINIEL MARIKI** Deceased, who died at 28th on the December day of 2021 and probate of whose (or letters od administration of whose estate) was granted to me by the ( court) 21st on the February day of 2022, are hereby required to send their claims to me at the following address within 60 days from the date of publication of this notice at the expiration of which time I shall proceed to hand over the assets to persons entitled thereto having regard only to the claims of which I shall then have had notice

**LILIAN FARES CHONJO**
**PO BOX 4523**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA TEMEKE**
**DAR ES SALAAM**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JOHN FRANK MWALONGO** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC 430 CGK** , CHASSIS NAMBA: **MD6M16PA4E03748,** ENGINE NAMBA: **AK4EK4603482.** Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: NJ/TR/RB/367/22**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

**HABARI KIMATAIFA**

# Rassia yalipua ghala la silaha

**MOSCOW,** Russia

WIZARA ya ulinzi ya Russia, imesema kuwa imeharibu silaha nyingi na zana zingine za kijeshi katika eneo la Donetsk, zikiwamo baadhi zilizotumwa kutoka Marekani na Ulaya.

Taarifa hiyo ilisema makombora ya angani yalipiga karibu na kituo cha reli cha Udachne, na kuteketeza vifaa ambavyo viliwasilishwa kwa vikosi vya Ukraine.

Hata hivyo, Shirika la habari la Uingereza (BBC) halikuweza kuthibitisha madai hayo, lakini ikiwa ni kweli, itakuwa pigo kwa Ukraine, ambayo inakabiliwa na athari katika eneo la mashariki la Donbas, ambako Russia ina silaha nyingi.

**Russia inaweza kupata wanajeshi wake 40,000 waliopoteza maisha tayari kufikia mwezi Juni. Katika vita vingine miongo mingi wamepoteza sana.**

**UKRAINE YATOA WITO WA KUZUIA ANGA**

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ametoa wito wa kuwekewa kwa mifumo ya kisasa ya ulinzi wa makombora kwa nchi yake akisema kuwa zaidi ya makombora 2,600 yametua nchini mwake tangu kuanza kwa uvamizi huo.

Alisema mifumo inayohitajika kwa sasa ni ile ya Iron Dome wa Israeli na American Patriot batteries wa Marekani.

Makombora ya masafa marefu ya Russia yamekuwa yakirushwa kuelekea Ukraine tangu kuanza kwa vita hivyo, wakati mengi yamedunguliwa, lakini zaidi yamefanikiwa kutua nchini humo.

Alisema wanahitaji sana mifumo zaidi ya silaha, huku mapigano katika eneo la mashariki la Donbas yakiendelea.

Mapigano ya Severodonetsk yamegeuka kuwa vita vya umwagaji damu mitaani, na hasara zimeripotiwa pande zote mbili.

Miongoni mwao ni mwanajeshi wa zamani wa Uingereza, aliyeuawa Ijumaa iliyopita.

Mshauri wa Rais Zelensky, alitoa pongezi kwa Jordan Gatley, akisema "alikuwa shujaa wa kweli.

Mykhailo Podolyak alisema siku zote watakumbuka mchango wake katika ulinzi wa Ukraine na ulimwengu huru. Katika hatua nyingine, Rais Zelensky alisema Russia ilikuwa inapeleka makuruti walio na mafunzo duni na wale waliokusanywa kwa uhamasishaji wa siri katika eneo la mashariki la Donbas.

Kulingana na kiongozi huyo, Russia inapeleka vikosi vya akiba huko Donbas kusaidia shambulio lake kwenye jiji la Severodonetsk, ambako kunaendelea kushuhudia mapigano makali.

"Russia inaweza kupata wanajeshi wake 40,000 waliopoteza maisha tayari kufikia mwezi Juni. Katika vita vingine miongo mingi wamepoteza sana," alisema.

Kwa mara nyingine tena alitoa wito kwa viongozi wa dunia kuipatia nchi yake mifumo ya kisasa ya kujikinga na makombora, akitaja majeruhi wa shambulio la hivi punde la kombora magharibi mwa Ukraine.

Gavana wa jimbo hilo, Serhiy Haidai, alisema bado vita vinaendelea katika eneo la Severodonetsk, hali inazidi kuwa ngumu baada ya jeshi la Russia kuharibu daraja la pili kuingia katika mji huo.

Alisema uharibifu wa daraja hilo ambalo linatumika kuingia Lysychansk, ni mkakati wa Russia kukata mawasiliano na kuteka mji wa Severodonetsk kwa haraka.

"Tayari haupitiki, kwa sasa wanaendelea kushambulia daraja la mwisho la tatu. Kama ninavyoelewa, wanataka kuukata mji huo ili kutowezesha uokozi wa watu kufanyika, au kuleta usaidizi," alisema Haidai. **BBC**



Wananchi wa maeneo ya Rushuru wakikimbia mapigano kati ya wanajeshi wa serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na waasi wa M23 Juzi. **PICHA: AFP**

## Rufani kupinga usafirishaji wahamiaji kusikilizwa

**LONDON,** Uingereza

MPANGO wa kuwapeleka nchini Rwanda waomba hifadhi wa Uingereza, upo mashakani baada ya mahakama kusubiriwa kutoa uamuzi wa kukubali au kukataa.

Mahakama ya Rufani inatazamiwa kuamua ikiwa itaruhusu ndege ya kwanza iliyogharamiwa na Ofisi ya Mambo ya Ndani ya Uingereza kwenda Rwanda ikiwa na watu wanaotafuta hifadhi.

Wanaharakati na wahamiaji walishindwa kupata zuio dhidi ya sera ya serikali katika Mahakama Kuu.

Lakini inadhaniwa idadi inayokabiliwa na kuondolewa hadi mji mkuu wa Rwanda wa Kigali siku ya Jumanne, imepungua sana.

Uingereza ilisema kuwasafirisha baadhi ya waomba hifadhi wanaofika kinyume cha sheria hadi nchini Rwanda kutadhoofisha magenge ya magendo yanayojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu.

Rufani hiyo imekatwa na Muungano wa Huduma za Umma na Biashara, ambao unawakilisha asilimia 80 ya wafanyakazi wa kikosi cha mipaka, pamoja na mashirika ya misaada Care4Calais na Detention Action.

Jana kesi tofauti pia ilitazamiwa kusikilizwa katika Mahakama Kuu Jumatatu, baada ya shirika lingine la kutoa misaada kwa wakimbizi, Asylum Aid, kuomba zuio la dharura la muda dhidi ya safari za ndege kuelekea taifa hilo la Afrika Mashariki. **BBC**

## 30,000 wakimbia mapigano Bunagana

**GOMA,** DRC

ZAIDI ya watu 30,000 wamekimbia makazi yao baada ya kuibuka mapigano kati ya vikosi vya serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na waasi wa M23.

Mapigano hayo makali yametokea katika maeneo ya Bunagana na viunga vyake katika eneo la Rutshuru katika jimbo la Kivu Kaskazini.

Kulingana na taarifa zilizotolewa na Umoja wa Mataifa, Baada ya mapigano hayo, mji wa Bunagana uko chini ya udhibiti wa vikosi vya serikali.

Taarifa hiyo ilisema zaidi ya watu 5,000 wametoroka eneo la Bunangana na viunga vyake na kuelekea Uganda.

Shirika la Msalaba Mwekundu la Uganda lilisema kuna haja ya msaada zaidi kwa wakimbizi waliovuka mpaka hadi siku ya Jumapili.

Msemaji wa M23 aliiambia BBC kwamba wanajeshi wengi wa FARDC waliuawa katika mapigano hayo na wengine walikimbia na silaha zao.

Alipoulizwa iwapo walikuwa wameukamata mji wa Bunagana, Willy Ngoma alisema: FARDC inadai kuwa imerudi nyuma na kuwasaka wapiganaji wa M23 ambao walivamia Bunagana na kuacha maiti kadhaa.

Taarifa iliyotolewa na FARDC, ilisema wakati wa mapigano hayo walisaidiwa na ndege za kivita za MONUSCO.

FARCD pia iliishutumu Rwanda kwa kuwasaidia M23 katika jaribio la kuiteka Bunagana, jambo ambalo serikali ya Rwanda imekuwa ikikanusha mara kwa mara. **BBC**

# MBEYA CITY YAZITAKA TENA POINTI 3 ZA SIMBA ALHAMISI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, ametangaza vita vya kuchukuwa pointi tatu zingine katika mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba.

Timu hizo zitakutana Juni 16, mwaka huu katika dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam huku Simba yenye pointi 51 ikiwa wenyeji wa mchezo huo baada ya ule wa awali ugenini jijini Mbeya, kuangukia kichapo cha bao 1-0.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema kikosi chake kimewasili salama jijini Dar es Salaam na tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo huo.**

Alisema wanaendelea kufanya maandalizi ya mwisho kuhakikisha wanakuwa bora zaidi ya wapinzani wao ili kupata matokeo mazuri katika mchezo huo.

"Tumefanyia kazi madhaifu yetu, lakini ubora wa Simba, hatuwadharau hata kidogo wapinzani wetu kwa sababu ni timu nzuri na ina wachezaji bora," alisema Lule.

Alisema licha ya Simba kutofanikiwa malengo yao ya kutwaa ubingwa anaamini watakuja kivingine ili kuhakikisha wanashinda mechi zilizobaki, jambo ambalo nao wanajipanga ili kuhakikisha wanapata pointi nyingine kwa Simba.

Mbeya City ilipata pointi tatu katika mchezo wa duru la kwanza kwa kuibuka na ushindi wa bao 1-0, lililofungwa na Paul Nonga, mchezo uliopigwa katika Dimba la Sokoni, Mbeya.

Mbeya City ipo katika nafasi ya kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 32 baada ya kushuka dimbani mara 26 msimu huu.

**MABINGWA...**



Wachezaji wa timu ya Tegeta United wakikabidhiwa kombe na Meneja Uhusiano wa SelCom, Bella Hakili, baada ya kuibuka washindi kwenye mashindano ya Dar Youth Cup yaliyohusisha vijana wenye umri wa chini ya miaka tisa, 11 na 13 kutoka timu mbalimbali yakiwa na lengo la kuibua na kuendeleza vipaji vya soka nchini. Mashindano hayo yaliyofanyika mwishoni mwa juma katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Djuma, Lusajo vinara wa 'assists' Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa kulia wa Yanga, Djuma Shaaban, straika wa Namungo Reliants Lusajo na Paul Buswita wa Ruvu Shooting, wanaongoza kwa kupiga pasi zilizozaa mabao 'assists' mpaka sasa wakati huu Ligi Kuu Tanzania Bara ikiingia raundi ya 27.

Wachezaji hao kila mmoja ametoa 'assists' tano, ambazo ndiyo takwimu za juu kwenye ligi hiyo mpaka sasa.

Wakati Djuma ni beki wa pembeni, washindani wenzake katika mbio hizo ni mastraika.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu hadi kufikia raundi ya 26, wanaofuatia ni Tepsi Evance wa Azam FC, Victor Akpan wa Coastal Union, Shomari Kapombe wa Simba, Christian Zigah wa Biashara United, na Aboubakar Ngalema wa Dodoma Jiji ambao wote wana 'assists' nne kila mmoja mpaka sasa.

Katika hatua nyingine, mchezaji wa Mbeya City, Frank Ikobela anaongoza kwa kuonyeshwa kadi nyingi za njano kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, akiwa ameshaonywa mara nane.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, anafuatiwa na Salum Salum wa Biashara United na Abdallah Hamad wa KMC ambao wana kadi saba za njano mpaka kufikia raundi ya 26.

Wachezaji wanane wanashika nafasi ya tatu kwa kutwangwa kadi nyingi, wote wakiwa na kadi sita kila mmoja.

Wachezaji hao ni Hashim Manyanya na Haruna Shamte wote wa Namungo, Stephen Duah wa Kagera Sugar, Kassim Haruna wa Polisi Tanzania, Sospeter Bajana wa Azam FC, Ally Kombo wa Ruvu Shooting, Salmin Hoza kutoka Dodoma Jiji na Mubarak Hamza wa Coastal Union.

## Deo Kanda sasa ruksa Mtibwa Sugar

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa zamani wa Simba na TP Mazembe, Deo Kanda, hatimaye amepata leseni ya kuitumikia klabu ya Mtibwa Sugar kwenye mechi zilizosalia za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nyota huyo sasa ameruhusiwa kuichezea timu hiyo, baada ya sakata la muda mrefu dhidi ya timu yake ya TP Mazembe, lakini baadaye tena klabu ya Kitayosce ikaingilia kati.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, amesema kwa mara ya kwanza mchezaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ataonekana uwanjani akiichezea Mtibwa baada ya kumaliza matatizo yaliyokuwa yanamkabili.

"Kwa sasa nitangaze rasmi kuwa Deo Kanda ataanza kuonekana na jezi ya Mtibwa Sugar baada ya yale matatizo ya muda mrefu kumalizika na amepata leseni ya kucheza," alisema.

Mchezaji huyo alisajiliwa na Mtibwa kipindi cha dirisha dogo la usajili akitokea TP Mazembe ya DR Congo, lakini timu hiyo ilikataa kutoa Uhamisho wa Kimataifa (ITC), kiasi cha kukaa muda mrefu bila kucheza, hivyo kuamua kupiga hodi FIFA ambao walitoa ruhusa ya mchezaji huyo kucheza.

Hata hivyo, Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilimzuia baada ya Kitayosce nayo kupeleka malalamiko kuwa nayo ilimsajili kipindi hicho hicho cha dirisha dogo.

Mtibwa iliamriwa kuirudishia Kitayosce pesa zao za usajili ili ipate ruhusa ya kumtumia mchezaji huyo, ambapo kwa sasa kila kitu kimetekelezwa.

Mchezaji huyo kwa mara ya kwanza alicheza Ligi Kuu Tanzania Bara akiwa na klabu ya Simba mwaka 2019 hadi 2020, akiitumikia miamba hiyo kwa mkopo kutoka TP Mazembe.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POBGA FRESH JUVE**

KLABU ya Juventus ina uhakika na matumaimi makubwa ya kumsajili, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29 bure kutoka Manchester United. Kiungo huyo Mfaransa amekubali kusaini mkataba wa miaka minne. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

**BERGWIJN TIMU KIBAO**

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Steven Bergwijn amesema anasakwa na klabu kadhaa wakati huu ambapo winga huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 24, akitaka kutimka. Ajax wako kwenye mazungumzo ya kumsajili msimu huu. ***(90min)***

**ERIKSEN KUTIMKA BRENTFORD**

KIUNGO wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30, ameamua kutafuta changamoto mpya na anajiandaa kutimka Brentford. Klabu za Tottenham Hotspur na Manchester United zinamendea nyota huyo. ***(Express)***

**ANTONY AFUKUZIWA UNITED**

MANCHESTER United wanamfukuzia winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 22 kutoka Ajax, na kiungo wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye miaka 25 kutoka Barcelona. ***(Talksport)***

**SLONINA HUYOOO CHELSEA**

CHELSEA wanakaribia kumnasa kipa Mmarekani Gabriel Slonina mwenye umri wa miaka 18, kutoka Chicago Fire baada ya ofa ya Real Madrid ya pauni milioni 8.5 kukataliwa. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

**CASTELLANOS AWANIWA LEEDS**

LEEDS United wanaongoza katika mbio za kumsaka mshambuliaji wa New York City mwenye miaka 23, raia wa Argentina, Valentin Castellanos. ***(Give Me Sport)***

**GUENDOUZI AMVUTA SALIBA**

KIUNGO Matteo Guendouzi anatarajia mlinzi William Saliba mwenye umri wa miaka 21, atafuata nyayo zake na kurejea Marseille kutoka Arsenal msimu huu baada ya wote kuwa kwa mkopo kwenye klabu hiyo ya Ufaransa msimu uliomalizika. ***(90min)***

**KOULIBALY ATAKIWA BARCA**

KAMA mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 23, ataondoka Sevilla na kujiunga na Chelsea, basi Barcelona itaelekeza nguvu zake kumsajili Kalidou Koulibaly, ingawa Napoli inaweza kutaka angalau pauni milioni 34.1 kwa ajili ya mlinzi huyo raia wa Senegal. ***(Mundo Deportivo)***

**DYBALA SAFI INTER**

INTER Milan inajiandaa kumsajili Paulo Dybala kwa uhamisho huru kutoka Juventus, na mshambuliaji huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 28, atasaini miaka mitatu. ***(Goal)***

**PSG YAKWAMA KWA SKRINIAR**

OFA ya Paris St-Germain ya pauni milioni 34.1 kwa ajili ya mlinzi wa Slovakia, Milan Skriniar imekataliwa, lakini Inter Milan wanaweza kukubali kuchukua pauni milioni 51.2 kwa ajili ya mlinzi huyo mwenye umri wa miaka miaka 27. ***(Gazzetta dello Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LIVERPOOL YAMALIZA KAZI RASMI USAJILI WA NUNEZ

●●● Asubuhi mapema Jumatatu (jana), Benfica iliweka wazi kuwa imemuuza kwa kiasi cha euro...

**LISBON,** Ureno

KLABU ya Benfica imethibitisha kuwa wamefikia makubaliano ya kumuuza mshambuliaji wao, Darwin Nunez kwa Liverpool kwa mkataba ambao unaweza kupanda hadi euro milioni 100.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, aling'ara nchini Ureno msimu uliopita, akipachika mabao 34 katika michezo 41 na hivyo kuzivutia klabu nyingi kubwa Ulaya.

Liverpool walilazimika kuelekea mbele ya foleni ya kuinasa saini yake, na baada ya mazungumzo magumu kuhusu ada yake ya uhamisho, hatimaye walifikia makubaliano wikendi hii.

**Sasa, Benfica wamethibitisha kuwa Liverpool watalipa euro milioni 75 ya awali ili kumsajili Nunez, na nyongeza ya euro milioni 25.**

"Asubuhi mapema Jumatatu (jana), Benfica iliifahamisha Tume ya Soko la Usalama la Ureno kwamba, imefikia makubaliano na Liverpool FC kwa mauzo ya haki zote za mchezaji Darwin Nunez, kwa kiasi cha euro milioni 75," ilisema taarifa ya klabu hiyo kwenda kwenye vyombo vya habari.

"Kwa Tume ya Soko la Usalama, Benfica pia iliarifu kwamba, makubaliano hayo yanatoa malipo ya kiasi tofauti, kwa hiyo kiasi cha jumla cha mauzo kinaweza kufikia euro milioni 100.

"Imefahamika zaidi kwamba, makubaliano yaliyotajwa hapo juu yanategemea kusainiwa kwa mkataba wa ajira wa mchezaji huyo kuwa mali rasmi ya Liverpool FC."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 253,

MECHI KALI
GERMANY
VERSUS
ITALY
1 | 1.80
X | 3.55
2 | 4.27

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KOCHA SENEGAL ATAKA MANE AJIUNGE BAYERN




**DAKAR,** Senegal

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Sadio Mane, amehimizwa kusajiliwa na Bayern Munich na kocha wake wa timu ya Taifa ya Senegal, Aliou Cisse.

Mane amekuwa akihusishwa sana na kuhamia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, huku ikiwa imebakia miezi 12 tu kumaliza mkataba wake wa sasa pale Anfield.

Klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England inasemekana kukataa ofa mbili za Bayern kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye ametwaa mataji sita makubwa katika misimu nane akiwa na 'Wekundu' hao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal, alidokeza kutaka kuhama akiwa kwenye majukumu ya kimataifa, na Cisse anaamini kuwa Bayern ndiyo chaguo bora zaidi kwa maisha ya Mane ikiwa anataka kuondoka Liverpool.

"Ninawaambia vijana wangu wajaribu kusuluhisha masuala ya mikataba yao ili ligi zao zitakaporejea wawe tayari wamepata msingi bora," alisema Cisse akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilisikia kuhusu Sadio kutakiwa Bayern. Kwangu mimi, ni klabu ambayo ina hadhi yake. Bayern ni timu bora na pale ndio panapomfaa Mane.

"Sadio alicheza katika klabu ya Salzburg nchini Austria, ambayo ni nchi ya mpakani na Ujerumani, na hiyo inamaanisha kuwa haendi katika eneo asilolijua na lisilojulikana.



# Argentina, Brazil zapewa Kombe la Dunia 2022

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Hispania, Luis Enrique, amesema anazichukulia Argentina na Brazil ndizo zenye nafasi kubwa zaidi ya kubeba Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, baadaye mwaka huu.

Argentina ilinyanyua taji la Copa America mwaka jana kwa ushindi wa bao 1-0 kwenye fainali dhidi ya Brazil katika Uwanja wa Maracana, likiwa ni taji lao la kwanza la kimataifa tangu mwaka 1993.

Kikosi hicho kinachoongozwa na kinara Lionel Messi kiliendeleza mafanikio hayo mapema mwezi huu kwa kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Italia katika Finalissima (inayokutanisha bingwa wa Copa America na bingwa wa Ulaya).

Timu hizo mbili za Amerika Kusini zilitoka sare katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia, ingawa Brazil ilimaliza kwa pointi sita mbele ya Argentina kwenye jedwali la kufuzu.

"Naziona Argentina na Brazil zikiwa juu ya timu nyingine zote," alisema Luis Enrique akiwaambia waandishi wa habari Jumamosi.

"Ndio kuna timu nyingi, lakini nikiangalia viwango vya timu nyingine, Argentina na Brazil ziko juu zaidi na zina nafasi kubwa sana ya kufika fainali ya kubeba kombe mwaka huu.

## HABARI MICHEZO

,545,950

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/06/22 | 21:00 | Plaza Colonia CD vs CA Boston River | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 02. 14/06/22 | 21:00 | San Lorenzo vs Arsenal Sarandi | 2.34 | 2.95 | 3.00 |
| 03. 15/06/22 | 01:00 | Patronato Parana vs Aldosivi | 2.31 | 3.10 | 2.91 |
| 04. 15/06/22 | 03:30 | Juventude RS vs Santos | 2.27 | 2.89 | 3.18 |
| 05. 15/06/22 | 20:00 | Barracas Central vs Union Santa Fe | 2.45 | 3.04 | 2.75 |
| 06. 15/06/22 | 22:30 | Atletico Tucuman vs Lanus | 2.43 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 15/06/22 | 22:30 | Banfield vs Central Cordoba | 2.21 | 3.04 | 3.14 |
| 08. 16/06/22 | 03:30 | Atletico Pr vs Corinthians | 2.24 | 2.90 | 3.24 |
| 09. 16/06/22 | 03:30 | America Mineiro MG vs Fluminense | 2.35 | 3.10 | 3.00 |
| 10. 16/06/22 | 22:15 | Keflavik IF vs Stjarnan | 2.70 | 3.48 | 2.26 |
| 11. 16/06/22 | 23:15 | Valur vs Breidablik | 2.61 | 3.44 | 2.35 |
| 12. 17/06/22 | 03:30 | CA Platense vs Gimnasia y Esgrima | 2.66 | 3.00 | 2.56 |
| 13. 17/06/22 | 03:30 | Racing Club vs Velez Sarsfield | 2.36 | 3.10 | 3.00 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 14/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3583 | South Korea vs Egypt | 1.61 | 3.68 | 5.93 |
| 14:30 | 5281 | Afghanistan vs Cambodia | 1.41 | 4.14 | 6.70 |
| 15:00 | 1978 | CA River Plate (Arg) vs Colon de Santa Fe Reserve | 1.82 | 3.50 | 4.10 |
| 15:00 | 4499 | Maldives vs SRI Lanka | 1.73 | 3.34 | 4.52 |
| 15:00 | 5802 | Arsenal FC Reserve vs San Lorenzo de Almagro Res. | 2.55 | 3.09 | 2.60 |
| 16:00 | 2912 | Malaysia vs Bangladesh | 1.14 | 5.88 | 19.61 |
| 16:00 | 3581 | Etincelles vs Gasogi United | 2.66 | 2.81 | 2.71 |
| 16:00 | 4785 | Wolkite City FC vs Mekelakeya | 2.90 | 2.80 | 2.65 |
| 17:00 | 1966 | CA Lanus vs Atletico Tucuman Reserve | 1.80 | 3.60 | 4.00 |
| 17:00 | 4433 | Huracan Reserve vs Defensa Y Justicia Reserve | 2.35 | 3.05 | 3.05 |
| 17:00 | 5178 | CA Central Cordoba SE Reserve vs Banfield Reserve | 3.06 | 3.11 | 2.22 |
| 18:00 | 1627 | HJS Akatemia vs Haka | 14.66 | 7.43 | 1.11 |
| 18:00 | 3919 | India vs Hong Kong | 2.16 | 3.09 | 3.19 |
| 18:00 | 5035 | Kyrgyzstan vs Tajikistan | 1.97 | 3.05 | 3.79 |
| 18:30 | 1462 | Japs vs AC Oulu | 7.05 | 4.70 | 1.34 |
| 18:30 | 2804 | Uzbekistan vs Thailand | 1.30 | 4.62 | 8.85 |
| 18:30 | 4572 | Lahti vs Atlantis FC | 1.11 | 7.43 | 14.66 |
| 18:30 | 5521 | Italy U21 vs Ireland U21 | 1.41 | 4.41 | 6.08 |
| 19:00 | 1201 | Norway U21 vs Azerbaijan U21 | 1.08 | 7.85 | 21.59 |
| 19:00 | 3820 | Club A Bizertin vs US Ben Guerdane | 2.89 | 3.14 | 2.29 |
| 19:00 | 4851 | Armenia vs Scotland | 6.03 | 3.87 | 1.55 |
| 19:00 | 4962 | Moldova vs Andorra | 1.57 | 3.69 | 6.26 |
| 19:00 | 5103 | Denmark U21 vs Turkey U21 | 1.50 | 4.23 | 5.12 |
| 19:00 | 5299 | Wales U21 vs Gibraltar U21 | 1.01 | 11.82 | 49.26 |
| 19:15 | 4441 | Jordan vs Kuwait | 2.39 | 2.96 | 2.91 |
| 20:00 | 3816 | Taby FK vs Orebro Syrianska | 2.42 | 3.93 | 2.32 |
| 20:00 | 5155 | Eidsvold Turn vs Kongsvinger IL | 5.29 | 3.82 | 1.54 |
| 21:00 | 1560 | Afturelding Mosfellsbaer W vs IBV Vestmannaeyjar W | 7.68 | 6.10 | 1.24 |
| 21:00 | 2214 | Thor Ka Akureyri W vs KR Reykjavik W | 1.25 | 5.70 | 8.06 |
| 21:00 | 2324 | Costa Rica vs New Zealand | 1.69 | 3.14 | 5.30 |
| 21:00 | 2688 | Plaza Colonia CD vs CA Boston River | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 21:00 | 4288 | San Lorenzo vs Arsenal Sarandi | 2.33 | 3.00 | 2.95 |
| 21:45 | 1301 | Liechtenstein vs Latvia | 8.71 | 4.96 | 1.33 |
| 21:45 | 1332 | Turkey vs Lithuania | 1.07 | 9.72 | 28.35 |
| 21:45 | 1956 | Poland vs Belgium | 3.33 | 3.38 | 2.11 |
| 21:45 | 2288 | Germany vs Italy | 1.80 | 3.55 | 4.27 |
| 21:45 | 2374 | ES Setif vs NA Hussein Dey | 1.20 | 5.47 | 11.73 |
| 21:45 | 2575 | England vs Hungary | 1.31 | 4.81 | 10.18 |
| 21:45 | 2951 | Netherlands vs Wales | 1.32 | 5.04 | 8.68 |
| 21:45 | 5061 | Romania vs Montenegro | 1.90 | 3.24 | 4.25 |
| 21:45 | 5423 | Bosnia and Herzegovina vs Finland | 2.01 | 3.27 | 3.73 |
| 21:45 | 5465 | Ukraine vs Ireland | 1.82 | 3.44 | 4.35 |
| 21:45 | 5693 | Luxembourg vs Faroe Islands | 1.46 | 4.03 | 7.26 |
| 22:00 | 1808 | French Guiana vs Belize | 1.25 | 5.10 | 9.82 |
| 22:15 | 3449 | Indonesia vs Nepal | 1.09 | 7.07 | 24.54 |
| 22:15 | 3879 | Keflavik W vs Stjarnan W | 9.83 | 6.09 | 1.20 |
| 22:15 | 4567 | UMF Selfoss W vs Valur Reykjavik W | 6.48 | 4.71 | 1.36 |
| 23:00 | 5703 | Bonaire vs Virgin Islands | U.s. | 1.38 | 4.43 |
| 23:15 | 1506 | Throttur Reykjavik W vs Breidablik Kopavogur W | 5.86 | 4.79 | 1.39 |
| 23:30 | 1972 | Turks And Caicos Islands vs Sint Maarten | 5.69 | 4.32 | 1.44 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# KIYANGA WA TEMBO WARRIORS ATWAA KIATU MICHUANO ULAYA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya soka la Watu wenye Ulemavu (Tembo Warrior), Alfan Kiyanga ameibuka mfungaji bora, kwenye mashindano ya Ulaya yalimalizika juzi nchini Poland.

**Tembo Warriors ilishiriki michuano hiyo kama timu alikwa, ikiitumia kujiandaa na Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchi ni Uturuki.**

Katika michuano hiyo, Tembo Warriors ilishika nafasi ya tano huku Kiyanga anayecheza soka la kulipwa nchini Uturuki katika Klabu ya Yeditepe, akiondoka na tuzo ya mfungaji bora baada ya kufunga mabao sita katika mechi tatu alizocheza.

Tanzania na Morocco zilikuwa nchi pekee alikwa kutoka barani Afrika na zote zilikuwa katika Kundi A pamoja na mwenyeji, Poland.

Akizungumza na gazeti hili jana, kocha wa timu hiyo, Ivo Mapunda, alisema mashindano hayo yamewapa mwanga mzuri wa kuona mapungufu yao kuelekea maandalizi ya michuano ya Kombe la Dunia.

Alisema licha ya kutopata matokeo mazuri na kumaliza katika nafasi ya tano, lakini mashindano hayo yamesaidia kuona mapungufu ya kikosi chake kuelekea katika maandalizi makubwa ya Fainali za Kombe la Dunia.

"Hii michuano imetusaidia sana kuona ubora na madhaifu ya kikosi cha timu yetu hasa kipindi ambacho tuko katika maandalizi ya kujiandaa na michuano ya Kombe la Dunia," alisema Mapunda.

Alisema Tembo Warriors kwenda kushiriki katika michuano hiyo ni kipimo kizuri kabla ya mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika Oktoba mwaka huu nchini Uturuki.



Straika wa Timu ya Taifa ya Tanzania ya soka la Watu wenye Ulemavu (Tembo Warrior), Alfan Kiyanga akionyesha tuzo aliyokabidhiwa baada ya kuibuka mfungaji bora kwenye mashindano ya Ulaya yalimalizika juzi nchini Poland. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Kipanga, Chipukizi dimbani Ijumaa Fainali Kombe la FA*

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MCHEZO wa Fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu FA Cup, unatarajiwa kupigwa Ijumaa wiki hii katika Uwanja wa Amaan Kisiwani Unguja.

Mchezo huo utaikutanisha miamba ya soka visiwani hapa, Maafande wa Jeshi la Wananchi, timu ya Kipanga dhidi ya Chipukizi kutokea Kisiwani Pemba. Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Bakari 'Cheupe', alisema maandalizi yote kuelekea mchezo huo yamekamilika, hivyo kilichobaki ni mashabiki kujitokeza kwa wingi uwanjani kushuhudia mchezo huo.

Alisema timu ya Chipukizi itawasili Unguja kesho, Jumatano ikitokea Pemba kwa ajili ya mchezo huo wa fainali ambao unasubiriwa kwa hamu na wadau wa soka hapa Zanzibar.

Alisema bingwa wa michuano hiyo atajinyakulia kitita cha shilingi milioni 30 kutoka kwa wadhamini Wakuu wa Ligi Kuu Zanzibar, Benki ya Watu wa Zanzibar pamoja na kukata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, CAF.

Wakati huo huo Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Hashim Salum Hashim, alisema kwa upande wa Ligi Kuu Zanzibar, mchezo wa mwisho wa kukabidhi Kombe la Ubingwa kwa KMKM ambayo itacheza dhidi ya Mlandege, utapigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Amaan.

Alisema mchezo huo ndio utakaokwenda kufunga rasmi pazia la Ligi Kuu Zanzibar katika msimu huu wa 2021/22.

# Michezo

Jumanne Juni 14, 2022

Nipashe



Liver yamaliza kazi kwa Nunez

UKURASA 21

ANACHEEEKA...



Moses Phiri (kushoto) na mchezaji mwenzake wa Zanaco akishangilia moja kati ya mabao aliyoifungia timu yake msimu huu. **PICHA: MTANDAO**

## Faridi afungwa Yanga, yaanika wakimataifa

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umetangaza kufanya usajili wa wachezaji wanne wa kigeni kwa ajili ya kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu mpya huku ukimwongezea mkataba wa miaka miwili winga wao, Faridi Mussa.

Akizungumza jijini jana, Msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara, hakuwa tayari kutaja majina ya wachezaji wanaowasajili wa kimataifa, lakini alizitaja nchi wazotaka nyota hao kuwa ni Afrika Kusini, Ivory Coast, Angola na ndani ya Ukanda huu wa Afrika Mashariki.

"Tutafanya usajili wa wachezaji wa kimataifa wanne, huwa hatusajili kwa tetesi tunasajili kwa uhakika kwa uhakika sisi ni klabu kubwa," alisema Manara.

Alisema msimu huu wanataka kusajili wachezaji ambao wataleta ushindani kwenye kikosi chao ambacho mpaka sasa hakijapoteza mchezo hata mmoja.

Licha ya kutowataja majina, wachezaji ambao wanahusishwa na klabu hiyo ni kiungo mshambuliaji Stephane Aziz Ki wa Asec Mimosas ya Ivory Coast na Lazarous Kambole kutoka Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Kuhusu mchezo wao wa kesho dhidi ya Coast Union ya Tanga utakaopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, alisema wanaendelea kujifua kwa ajili ya mchezo huo ambao wanakwenda kuutangaza ubingwa kwa kupata pointi tatu.

# Phiri, Simba imeisha hiyo

## ●●● Atua rasmi kuunda 'kombinesheni' na Wazambia wenzake Chama na Bwalya, huku...

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wameendelea kukisuka kikosi chao kimyakimya kuelekea msimu ujao wa 2022/ 23, na tayari wamemaliza kazi kwa mshambuliaji wa Zanaco ya Zambia, Moses Phiri, imefahamika.

**Licha ya Klabu ya Simba kuendeleza utamaduni wake wa kutaka kuwatangaza wachezaji wanaowasajili kwa utaratibu maalum pindi dirisha la usajili litakapofunguliwa, lakini Nipashe limepata taarifa za uhakika kuhusu mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara, kumalizana na Phiri.**

Phiri ambaye anatisha kupachika mabao, amejiunga na Simba kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Zanaco na rasmi ataanza kuvaa jezi nyekundu na nyeupe Simba msimu ujao.

Chanzo chetu cha uhakika ndani ya klabu hiyo kimemweleza mwandishi wetu kuwa mshambuliaji huyo amemalizana na Simba licha ya wapinzani wao, Yanga nao awali kutaka kuingilia dili hilo.

"Simba ilishakubaliana na Phiri tangu usajili wa dirisha dogo, lakini dili hilo lilishindikana kutokana na klabu yake kukabiliwa pia na michuano ya kimataifa, hivyo haikuwa tayari kumwachia kwa wakati huo," kilieleza chanzo chetu huku kikiomba hifadhi ya jina lake.

"Hata hivyo, wapinzani wao...nao walitaka kumsajili lakini waligonga mwamba baada ya kutajiwa dau kubwa, lakini mchezaji mwenyewe alionyesha kuwa na mapenzi zaidi na Simba."

Lakini katika Wikipedia ya Phiri, nayo inaonyesha klabu yake ya sasa ni Simba Sports Club.

Phiri mwenye umri wa miaka 29, sasa ataungana na nyota wenzake wawili kutoka Zambia ndani ya kikosi cha Simba, viungo Rally Bwalya na Clatous Chama ambao wote wanaichezea timu yao ya taifa.

Katika kile kinachoonekana hawataki mipango yao kuingiliwa, mwishoni mwa wiki Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', baada ya tetesi nyingi za usajili kuvuma huku wakidaiwa kuzidiwa ujanja na watani wao, Yanga katika mbio za kumsajili kiungo mshambuliaji wa Asec Mimosas ya Ivory Coast, Stephane Aziz Ki, alisema kwa sasa mambo yao ya usajili wanayapeleka kimyakimya.

"Tumejifunza kuwa na weledi mkubwa kwenye usajili, maana wapinzani wetu, Al Ahly, Orlando, Berkane wanafuatilia kila tunapopiga hodi. Sasa kama tutakuwa tunatembea na kamera kupiga picha na wachezaji tunaowafuatilia, itakuwa shida, wanachama na mashabiki wa Simba tuachieni sisi kazi ya kusajili," alisema.

Rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Dk. Mohammed "Mo" Dewji, tayari ametangaza kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya usajili ili kukiimarisha kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu ujao wa michuano iliyopo mbele yao hususan Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbali na usajili wa wachezaji, Simba pia ipo katika harakati za kusaka kocha mpya baada ya kumtimua kazi Kocha Mkuu, Mhispania Pablo Franco kwa kile kilichoelezwa ni kushindwa kufikia malengo aliyowekewa ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu, Kombe la FA na kufika nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >